



**ZANZIBAR** kuja kivingine uwekezaji visiwa 2024

UKURASA 4



**WASTAAFU** wamwangukia Rais nyongeza pensheni

UKURASA 7




# Nipashe

Jumatatu Januari 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581542

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz  www.facebook.com/nipashetz  www.instagram.com/theguardian_newspaper


## SALAMU ZA MWAKA MPYA

# Rais Samia, Mwinyi wajivunia mafanikio

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi

UKURASA WA 23

## SINGIDA FG, APR, SIMBA VITANI MAPINDUZI CUP LEO

MTIFUANO mkali unatarajiwa kushuhudiwa leo katika michuano ya Kombe la Mapinduzi wakati 'Wakulima wa Alizeti', Singida Fountain Gate, watakaposhuka Uwanja wa Amani Complex visiwani hapa kuvaana na Miamba ya Soka ya Rwanda, APR FC.

Mchezo huo utapigwa majira ya saa kumi alasiri wakati saa mbili usiku JKU SC wataikaribisha...

## Mtuhumiwa mauaji shambulio la visu 25 anaswa akitorokea nchi jirani

UKURASA 4

# Mbowe, kina Mdee uso kwa uso

UKURASA 2

**MICHEZO** KIPRE JUNIOR MCHEZAJI BORA DESEMBA UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Samia: 2023 uliimarisha ulinzi, usalama, udhibiti mfumuko bei

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema katika mwaka 2023 serikali inajivunia mafanikio mbalimbali iliyoyafikia mojawapo ikiwa kuimarika kwa ulinzi na usalama, kudhibiti mfumuko wa bei pamoja kukuza Pato la Taifa.

Aliyasema hayo wakati akitoa salamu za Mwaka Mpya kwa Watanzania kupitia vyombo mbalimbali vya habari na kusema kuwa licha ya kuwapo matatizo ya kiuchumi yaliyotokana na athari za UVIKO-19 na vita ya Ukraine na Urusi, uchumi wa taifa ulizidi kuimarika.

**ULINZI, USALAMA**

Rais Samia alisema mwaka 2023 unaagwa nchini ikiwa na ulinzi na usalama unaoendelea kuimarika, mipaka yote ya nchi ikiwa salama huku vikosi vya ulinzi na usalama vikiwa imara.

"Sote tulishuhudia namna vikosi vyetu vilivyojitoa katika uokoaji na kurejesha hali ya kawaida pale tulipopatwa na maafa. Nitumie fursa hii kuvipongeza kwa ujasiri na uzalendo wao. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza wananchi kwa kuendelea kudumisha amani na umoja wa kitaifa," alisema.

Alisema licha ya changamoto za kiuchumi zilizoikumba dunia kutokana na ugonjwa wa UVIKO -19 na vita ya Ukraine na Urusi, nchi imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei, katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2023 ulipungua hadi wastani wa asilimia 3.9, ikilinganishwa na asilimia 4.3 kipindi kama hicho, mwaka juzi.

Pia ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa kwa mwaka 2023 ulikadiriwa kuongezeka kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2022 huku deni la taifa likiendelea kuwa himilivu.



Ukusanyaji wa kodi, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2023 ulifika Sh. trilioni 22.6, ikiwa ni ongezeko la asilimia nane ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2022.

Rais Samia alisema katika kuendelea kukuza na kuimarisha uchumi serikali imeongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 751 mwaka jana 2022 hadi Sh. bilioni 970 mwaka huu, sawa na ongezeko la asilimia 29.

Upande wa madini, alisema serikali imeendelea kutoa kipaumbele na mwaka jana kumekuwapo ongezeko la asilimia 6.43 la thamani ya madini yaliyozalishwa na ongezeko la asilimia 5.8 yaliyouzwa nje ya nchi hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.15.

Kwenye sekta ya utalii, alisema kwa kipindi cha Oktoba mwaka jana hadi Oktoba 2023, watalii 1,750,557 waliingia nchini ikilinganishwa na 1,381,881 mwaka 2022.

**UCHUKUZI**

Rais Samia aliielekeza Wizara ya Uchukuzi kuhakikisha kuwa ifikapo mwisho wa Julai 2024, safari za treni kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma ziwe zimeanza.

Alisema amekuwa akisikia mabadiliko ya tarehe za kuanza kwa safari hizo, huku wananchi wakichoshwa na sababu zinazotolewa kila mara kuhusiana na mabadiliko hayo.

Alisema kwa kuzingatia kuwa uzalishaji na ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa unachochewa na miundombinu ya usafiri na mawasiliano, serikali iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa vipande vya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Morogoro hadi Makutupora vimefikia zaidi ya asilimia 90.

**NISHATI**

Alisema katika kukabiliana na upungufu wa umeme unaosababisha nchi kuingia katika mgawo, serikali ilifanya jitihada kubwa kutekeleza mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere.

Kwa mujibu wa Rais Samia, mtambo wa kwanza wa umeme huo unatarajiwa kuwashwa Februari 2024 na wa pili utawashwa Machi itakaotoa megawati 470.

"Ni imani yangu na serikali kwa ujumla kuwa, hatua hizi zitaleta ufumbuzi wa kudumu kwa suala la mgawo wa umeme nchini. Aidha, serikali inaendelea kuwekeza kwenye vyanzo vingine vya umeme kama vile gesi, jua, na upepo ili kuongeza uhakika wa umeme," alisema.

**SEKTA YA AFYA**

Alisema kwa mwaka 2023 serikali iliwekeza nguvu kubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini kwa kuajiri wataalamu 17,309 na kutenga Sh. bilioni 190.9 kwa ajili ya kununua dawa.

**MAJI**

Serikali ilifanya uwekezaji mkubwa na kukamilisha miradi 506 ikiwamo 436 ya vijijini na 70 ya mijini yenye uwezo wa kuhudumia wananchi 5,754,340 hali iliyosababisha kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma za maji hadi asilimia 88 mijini na 77 vijijini.

Alisema pia serikali imeongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 654 mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 731 mwaka huu na kuwafikia wanufaika 220,075 kutoka 198,105.

**USHIRIKIANO KIMATAIFA**

Nchi imefanya vizuri katika medani ya kimataifa kwa kushiriki mikutano na kupokea wageni mashuhuri kutoka nchi mbalimbali na kuiletea mafanikio ikiwamo fedha kwa ajili ya miradi ya usalama wa chakula, mawasiliano vijijini, ujenzi wa miundombinu na masoko, ujenzi wa vyuo na ajira.

**MAZINGIRA**

Katika kukabiliana na athari za kimazingira ikiwamo mafuriko na magonjwa yanayosababishwa na mvua ya El-Nino, Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais TAMISEMI wanapaswa kuchukua tahadhari kuzuia mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza pamoja na malaria kwa mwaka huu.

Alisema katika mwaka 2023 serikali iliongeza kasi ya utekelezaji wa falsafa ya 'R' nne ambayo ni Maridhiano, Mageuzi, Ustahimilivu na Kujenga Upya, kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kurejesha Tume ya Mipango.

## Mbowe, kina Mdee uso kwa uso

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akiwamo Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freeman Mbowe na Katibu John Mnyika jana walikutana uso kwa uso na wabunge wa viti maalum, Halima Mdee na Ester Bulaya.

Walikutana wakati wa ibada maalum ya harambee ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Usharika wa Nshara, mkoani Kilimanjaro.

Harambee hiyo ililenga kukusanya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza wa kanisa hilo, iliyoongozwa na Mkuu wa Kanisa hilo, Askofu Fedrick Shoo.

Wanasiasa hao wapo kwenye msuguano wa kisiasa tangu Novemba 27, 2020, baada ya Mdee, Bulaya na wabunge wanawake wengine 17 kuvuliwa uanachama na Kamati Kuu ya chama hicho kwa madai ya kwenda kuapishwa bungeni ilhali chama hicho hakikupeleka majina yao katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa ajili ya nafasi hizo.

Wanasiasa hao hawakukubaliana na uamuzi huo na kuamua kukata rufani kwenye Baraza Kuu la CHADEMA ambalo nalo lilitupilia mbali rufani hiyo na kubariki kuvuliwa uanachama.

Mei 11, 2022, Mdee na wenzake walipinga mahakamani uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kutupilia mbali rufani hiyo na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilibatilisha uamuzi wa baraza hilo.

Hata hivyo, katika harambee Mdee na Bulaya waliungana na waumini wengine wa kanisa hilo akiwamo Mbowe ambaye familia yake ilitoa shukrani.

Shangwe na vigelegele vilitawala zaidi wakati Askofu Shoo alipowatambulisha wanasiasa hao ikiwa ni ishara ya kuthamini uwapo wao katika eneo hilo.

Kukutana kwa wanasiasa hao kumeibua maswali kutoka watu mbalimbali, wengine wakihoji pengine ni ishara kuwa mambo yameanza kuwa mazuri kati yao.

# ...Mwinyi ajivunia mafanikio lukuki 2023

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amebainisha mafanikio ya kiutendaji iliyoyafikia serikali yake kwa mwaka 2023, ukiwamo ushirikiano kati ya asasi za kiraia, wanasiasa na wananchi.

Amesema ushirikiano huo umewawezesha kutekeleza mafanikio ya mipango ya kukuza uchumi na kuimarisha huduma za jamii.

Katika hotuba yake aliyoitoa jana, Dk. Mwinyi alibainisha hali hiyo imewavutia wadau mbalimbali na kuongeza kuungwa mkono na washirika wa maendeleo yakiwamo ya kimataifa, taasisi mbalimbali, balozi za nje na nchi marafiki.

Alisema mwaka 2023 wamepata mafanikio katika kuimarisha ukuaji wa uchumi, uimarishaji wa miundombinu, biashara na uwekezaji, huduma za jamii zikiwamo elimu, afya, majisafi na salama, umeme na uimarishaji wa demokrasia na utawala bora.

"Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wote, viongozi wa ngazi mbalimbali na watumishi wote wa serikali, viongozi wa dini na asasi za kiraia, sekta binafsi na washirika wetu wa maendeleo wa ndani na nje ya Tanzania kwa ushikiriano waliotupa na kuiwezesha serikali kutekeleza mipango yake ya maendeleo kwa mafanikio.

"Pia natoa shukrani maalum kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, viongozi na watendaji wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano waliotupa katika kufanikisha shughuli za serikali," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema mwaka uliopita, wameshuhudia mafanikio makubwa ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo uimarishaji wa miundombinu ya elimu kwa ujenzi wa shule mpya 62.

Mengine ni kukamilika na kuanza kutumika kwa hospitali mpya 10 za wilaya zenye vifaa vya kisasa na hospitali moja ya mkoa ya Lumumba katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ujenzi wa vituo vya wajasiriamali kila wilaya na kuwapatia mikopo nafuu, kuwawezesha wavuvi wadogo na wakulima wa mwani kwa kuwapatia mikopo na vifaa.

Alisema mafanikio mengine ni kuanza ujenzi wa barabara kuu yenye urefu wa kilomita 103.5 za ndani mjini na vijijini (275), mjini (100) na madaraja ya juu mawili (flyover) katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar.

Mengine ni kuanza kwa mradi wa ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani kwa hatua mbalimbali zikiwamo za miundombinu ya barabara, utengaji wa maeneo kwa shughuli mbalimbali na kuanza ujenzi wa nyumba za wananchi waliopisha utekelezaji wa mradi huo.

Alisema serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa miradi mikubwa ya majisafi na salama Unguja na Pemba ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Dk. Mwinyi alisisitiza mwaka 2024 wananchi waongeze mshikamano wa kudumisha amani na umoja.

## HABARI KITAIFA

# Matukio 7 yaliyoleta simanzi, furaha 2023

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI Tanzania ikiungana na mataifa mengine kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2024, matukio mazuri na mabaya yaliyotawala mwaka 2023 yatabaki katika kumbukumbu ya Watanzania.

Mwaka 2023 ulikuwa ni wa safari ndefu yenye milima na mabonde, furaha na huzuni.

Gazeti hili limeainisha matukio yaliyoibua hisia za watu na kuzungumziwa zaidi nchini kwa mwaka huo kwa kuzingatia yenye neema na huzuni.

### MAPOROMOKO HANANG'

Usiku wa kuamkia Desemba 3, mwaka huo ulibadilisha maisha ya wakazi wa maeneo ya Katesh na Gendabi, Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara baada ya kutokea kwa maporomoko ya matope, mawe na magogo na kusababisha vifo vya watu 89, huku 139 wakijeruhiwa.

Maporomoko hayo yaliyosababishwa na mvua kubwa pia yaliziacha kaya 107 zilizokuwa na wakazi 322 bila makazi na mali zao kupotea.

### VIFO WATANZANIA VITA HAMAS, ISRAEL

Oktoba 3, viliibuka vita kati ya wanamgambo wa Hamas kutoka Palestina na Israel ambavyo vilisababisha vifo kwa Watanzania wawili Joshua Mollel na Clemence Mtenga waliokuwa nchini Israel kujifunza kilimo kwa vitendo.

Vijana hao walipoteza mawasiliano na ubalozi wa Tanzania tangu Oktoba 7 pindi Hamas walipovamia Israel na kuteka mamia ya raia.

### UVUMI MAKAMU WA RAIS

Ni tukio lililozua mjadala la kutoonekana hadharani kwa Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango kwa takribani siku 40 hali iliyozua taharuki na mijadala katika mitandao ya kijamii.

Baadhi ya Watanzania wakiiomba serikali iwaeleze alipo mkuu huyo wa nchi.

Katika taharuki hiyo maneno mengi yalisemwa, wapo waliosema kuwa amekwenda nje ya nchi kutibiwa na waliomzushia kifo.

Hata hivyo taharuki hiyo ilizimwa Desemba 10, baada ya Dk. Mpango kuonekana akishiriki ibada ya Jumapili katika Kanisa la Parokia Mwenyeheri Maria Theresa Lendochowska, lililoko Dodoma.

### MKATABA DP WORLD

Juni 10, Bunge la Tanzania liliridhia ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Dubai katika uendeshaji na endelezaji wa maeneo ya bandari nchini, hatua iliyoibua hisia tofauti miongoni mwa Watanzania.

Baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa na wachumi waliunga mkono uamuzi huo na wengine wakipinga na kuishauri serikali kufanyia marekebisho baadhi ya vipengele vilivyomo kwenye mkataba huo baada ya kutoeleweka na kutaka uwe wazi kwa Watanzania.

### VIFO VYA WATU MAARUFU

Mwaka 2023 ulikuwa ni simanzi kwa Watanzania baada ya kutokea kwa vifo vya watu maarufu ambao waliacha pengo kubwa kutokana na mchango wao katika jamii.

Wa kwanza ni Waziri wa Mambo ya Ndani na Ushirikiano wa Kimataifa (mstaafu), Benard Membe, aliyefariki dunia Mei 12.

Kifo cha mwanadiplomasia huyo nguli kilichoelezwa kutokana na homa ya mapafu kiliibua majonzi kwa Watanzania wengi kutokana na mchango wake mkubwa alioutoa katika kipindi cha uongozi wake na uchechemuzi aliouleta katika siasa katika uchaguzi wa mwaka 2020 alipowania nafasi ya urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo.

Aprili 18, 2023, aliyewahi kuwa Mbunge wa Butiama mkoani Mara, Nimrod Mkono (80), alifariki dunia akiwa Marekani alikokuwa akitibiwa tangu mwaka 2018 kwa ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu.

Kifo cha Nimrod kiliacha majonzi makubwa hasa kwa wanachama wa CCM kwa walichoeleza kumpoteza kada mtiifu ambaye enzi za ubunge alifanya mambo makubwa ya maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo elimu.

Juni 8, mfanyabiashara maarufu na aliyewahi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Mkoa wa Kusini Unguja, Mohamed Raza, alifariki dunia.



Maporomoko Hanang'

Raza, alifahamika zaidi katika juhudi zake za kukuza michezo visiwani Zanzibar na vile vile, alijikita kwenye siasa na hatimaye kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini.

Julai Mosi, aliyekuwa Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega, alifariki dunia baada ya kupata ajali ya kugongwa na trekta alipokuwa shambani kwake Mbarali.

Julai 18, Jecha Salum Jecha, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), alifariki dunia. Alipata umaarufu baada ya kufuta Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 Zanzibar.

Novemba 10, CCM ilipata pigo lingine baada ya mwanachama wake, Zelothe Stepehen, kufariki dunia baada ya kukitumikia chama na serikali katika nafasi mbalimbali ikiwamo ya Ukuu wa Mkoa wa Rukwa.

Mei 18, mmiliki wa kituo cha habari cha mtandao maarufu uliokuwa ukitembelewa na watu wengi wa Lemutuz Super Brand, Willium Malecela, maarufu kama Lemutuz alifariki dunia baada ya kuugua maradhi ya moyo kwa muda mrefu.

Aidha Desemba 12, mtayarishaji wa video za muziki wa bongofleva na mtoto wa mhubiri wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, GeorDavie, Nic Davie maarufu Nisher alifariki dunia.

### NDEGE YA MIZIGO YA ATCL

Mwaka 2023 ulikuwa ni wa mapinduzi ya kibiashara nchini baada ya Juni 3, Rais Samia Suluhu Hassan kuongoza Watanzania kupokea ndege ya mizigo aina ya Boeng 767 -300 F ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) yenye uwezo wa kubeba tani 54 kwa wakati mmoja.

Kuletwa kwa ndege hiyo kumeondoa adha ya usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi na ya nje kuingia ndani na kupunguza gharama za usafirishaji.

Kwa Mujibu wa Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, uwapo wa ndege hiyo yenye uwezo wa kufanya safari kwa saa 10 bila kutua, utatoa fursa kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo kusafirisha mizigo yao.

### UTEUZI MAKONDA

Oktoba 22, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan alimteua, Paul Makonda kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

Makonda alichukua nafasi ya Sophia Mjema, ambaye aliteuliwa kuwa mshauri wa Rais (masuala ya wanawake, watoto na makundi maalum).

Makonda ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, uteuzi wa ukuu wa mkoa ulitenguliwa mwaka 2020 baada ya kujitosa kwenye kinyang'anyiro cha ubunge, Jimbo la Kigamboni.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya**
**DODOMA MJINI Kituo**
**Cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 102 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU BONIFACE. M. NYANDA WA AREA "A" KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA HELENA DAUDI MPAZI**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,

*Marehemu hakuacha wosia

*Futa isioyohusika

Imetolewa leo Tarehe 28 Mwezi 12 Mwaka 2023

..........................................

**HAKIMU**





The Management and Staff of The Guardian Limited wish you a successful New Year 2024.
We are very grateful for having you as our business partner.
Thank you for your valuable patronage.
Your trust is highly appreciated.

Subscribe today our News Paper
epaper.ippmedia.com

IPPmedia The Guardian Nipashe

NipasheTz @TheguardianTz01 theguardianltd epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com +255 745 700 710

HABARI KITAIFA

# Anayetuhumiwa shambulio la mauaji kuchoma visu 25 anaswa

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Polisi limemkamata, Lucas Tarimo, anayetuhumiwa kumuua mpenzi wake, Beatrice Minja kwa kumchoma visu 25 mwilini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, mtuhumiwa Tarimo alikamatwa akiwa amejificha katika Kijiji cha Jema, Kata ya Oldonyo, Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha akijiandaa kukimbilia nchi ya jirani.

Beatrice alifariki dunia Desemba 27, mwaka huu akiwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) Hospitali ya Rufani KCMC, alikokuwa akiuguza majeraha yanayodaiwa kutokana na kuchomwa visu 25 na mtuhumiwa.

Taarifa hiyo ilisema mtuhumiwa huyo alikamatwa juzi alfajiri akiwa anajiandaa kukimbilia nchi ya jirani.

Kamanda Misime alisema mtuhumiwa baada ya kuona mkono wa serikali unamfikia alikunywa sumu inayotumika kuua wadudu na amepatiwa huduma ya kwanza, yupo vizuri na taratibu za kisheria zinaendelea.

"Tunawashukuru wananchi wa kata hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliotoa kwa Jeshi la Polisi hadi kufanikiwa kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo ingawa baada ya kuona mkono wa serikali unamfikia alikunywa sumu inayotumika kuua wadudu. Mtuhumiwa amepatiwa huduma ya kwanza na yupo vizuri," alisema Misime.



Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime

Tukio hilo ambalo lilisambaa kwenye mitandao ya kijamii, limeelezwa kuwa Beatrice na Tarimo waliwahi kuwa katika uhusiano wa kimapenzi, lakini uliotawaliwa na migogoro hali iliyosababisha mwanamke huyo kujitenga na mtuhumiwa huyo na kwenda kuanza maisha yake upya.

Kabla ya mtuhumiwa kuondoka inadaiwa alimpora Beatrice Sh. milioni 10 zilizokuwa za mtaji wa biashara na pesa za ujenzi wa nyumba ya mama yake, tukio ambalo aliliripoti polisi.

Novemba 12 majira ya jioni, Beatrice akiwa na wanawake wawili walishambuliwa na mtuhumiwa na Beatrice alichomwa visu 25 maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Wasamaria wema walimpeleka Beatrice katika Hospitali ya Huruma na kupatiwa rufani kwenda KCMC ambako alilazwa hadi umauti ulipomfikia Desemba 27.

Beatrice alifanyiwa upasuaji mara mbili na kushonwa majeraha 20.

# Z'bar kuja kivingine uwekezaji visiwa 2024

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, amesema, amani na usalama katika nchi ndio chachu kwa wawekezaji wengi wa kigeni kuona visiwa vya Unguja na Pemba sehemu sahihi ya kuleta mitaji yao.

Aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi la mradi wa kisiwa cha Bawe (Bawe Island Cocoon by Collection) kitakachojengwa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano kikiwa ni miongoni mwa visiwa 16 serikali ilivyokodisha kwa wawekezaji.

Zuberi alisema mradi huo ni wa tatu kuwekezwa na wawekezaji kutoka nchi za Luxemberg na Italia.

Aidha, alisema uamuzi wa wawekezaji hao kuendelea kuwekeza nchini ni kutokana na uzuri wa visiwa pamoja na imani kubwa waliyonayo kwa serikali kwa sera zake nzuri zenye kutoa matumaini ya kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema amani, utulivu na usalama pamoja na mazingira mazuri ya kuwekeza ni matunda yatokanayo na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

"Nichukue nafasi hii kuwashauri wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wenye uwezo, kuwekeza hapa nchini na serikali kama inavyotueleza siku zote inaunga mkono jitihada za wawekezaji hawa kwa lengo la kuimarisha uchumi na ustawi wa jamii wa wananchi wa Zanzibar," alisema.

Alisema serikali imeamua kufuata sera ya uchumi wa buluu kama mpango mkuu wa maendeleo ya Zanzibar ambao unahusisha matumizi ya rasilimali za baharini na maeneo yaliyozunguka katika shughuli za kiuchumi.

Aidha, serikali imeamua kukodisha visiwa hivyo vidogo kwa ajili ya uwekezaji baada ya kuona vimekaa kwa muda mrefu bila ya kuendelezwa na kushindwa kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Aliwataka wananchi kutosikiliza maneno ya upotoshaji yanayofanywa na baadhi ya watu dhidi ya dhamira njema ya serikali ya ukodishwaji wa visiwa hivyo.

"Niwaombe wananchi wote hususan wale wanaoishi pamoja na wale wanaotumia visiwa hivi katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii kuendelea kutoa ushirikiano wa hali na mali kwa serikali na wawekezaji ili kufanikisha utekelezaji wa miradi hii kwa manufaa mapana ya nchi yetu," alisema.

Alisema Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni chombo cha kuwawakilisha wananchi kilichotunga sheria mpya ya uwekezaji visiwani humo ya mwaka 2023 pamoja na mambo mengine, sheria hiyo imeweka masharti kwa wawekezaji ili kulinda rasilimali zikiwamo visiwa vidogo.

Kadhalika, sheria imetoa fursa kwa ushiriki wa wananchi katika shughuli za uwekezaji ikiwamo, kupatiwa fursa za ajira kwa wananchi wanaozunguka miradi hiyo, wawekezaji kuchangia uendelezaji wa huduma za kijamii katika maeneo ambayo miradi hiyo inayofanyika pamoja na kutoa fursa za kipaumbele kwa wananchi kuuza bidhaa zao katika miradi hiyo.

Aliitaka wizara inayosimamia uwekezaji Zanzibar kusimamia vizuri utekelezaji wa sheria hiyo mpya ili iweze kuleta matunda yaliyokusudiwa kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema Zanzibar ina visiwa vidogo 20 na kati ya hivyo 16 vimeshakodishwa kwa wawekezaji na mtaji wa wake ni jumla dola milioni 384.5.

Akizungumzia mradi wa Kisiwa cha Bawe uliowekewa jiwe la msingi, Sharif alisema mwekezaji amewekeza dola milioni 38 na utakuwa na majengo 159 zikiwamo hoteli za kifahari unatarajiwa kufunguliwa Machi mwaka 2024 na utazinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwekezaji Wananchi Kiuchumi, Mudrik Ramadha Soraga, alisema mradi huo ndio pekee uliofikia asilimia 60 ikilinganishwa na visiwa vingine.

Alisema visiwa 16 vilivyokodishwa ni urithi na kuwataka wawekezaji kutunza mazingira kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mkurugenzi wa mradi wa Bawe, Injinia Charles Lwanda, alisema wamevutiwa kuwekeza miradi mikubwa Zanzibar kutokana na mandhari nzuri, pia hali ya amani na usalama na watahakikisha kuwa inawanufaisha wananchi wakiwamo wavuvi.

# Mil. 198/- kujenga vyoo vya shule, zahanati

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

SERIKALI imetoa Sh. milioni 198.7 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya vyoo na usafi wa mazingira katika shule ya msingi na zahanati Kijiji cha Rukwa, wilayani Songwe.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kijijini hapa, wananchi hao walisema kipo pembezoni mwa Ziwa Rukwa, kimekuwa kikikabiliwa na matatizo mengi ikiwamo ukosefu wa vyoo, uchakavu wa majengo ya shule na zahanati.

Leah Mwashilindi, mkazi wa kijiji hicho alisema hali ya miundombinu ya shule na zahanati ni taabani, wakati mwingine wagonjwa kupata maambukizi yanayosababishwa na vyoo chakavu.

Samwel Mtawa, alisema wanaona faraja baada ya ujenzi wa vyoo vya kisasa na maboresho ya miundombinu ya maji na usafi wa mazingira kufanyika.

Akizungumza kwa niaba ya Mganga Mfawidhi wilayani hapa, Dk. Lydia Kyumana, alikiri kuwapo na uchakavu wa miundombinu ya vyoo na majengo katika zahanati hiyo, akisema kwa sasa serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya ukarabati.

Alisema Zahanati ya Rukwa ilianza kutoa huduma Januari, 2020 ikiwa na watumishi wawili, ikiwahudumia wakazi 1,668 huduma za nje, upimaji maabara, huduma za mama na mtoto na ushauri nasaa.

Alisema zahanati hiyo ilipokea Sh. milioni 60 kutoka serikalini zilizojenga matundu saba ya vyoo vikiwamo vya watu wenye ulemavu, bafu na miundombinu ya majisafi na majitaka pamoja na kizimba cha kuchomea taka. Alisema hadi sasa wamebakiwa na akiba ya Sh. milioni 27.5.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Cecilia Kavishe, alisema kutokana na umuhimu wa zahanati hiyo anasimamia kwa ukaribu zaidi ili ujenzi ukamilike kwa wakati.

Aliongeza kuwa mbali na zahanati hiyo pia walipokea Sh. milioni 166.1 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili, ofisi, nyumba ya walimu na matundu matatu ya vyoo kwenye Shule ya Msingi Rukwa na tayari ujenzi upo hatua za mwisho.

Alisema hadi sasa Sh. milioni 144.3 zimetumika na wamebakiwa na akiba ya Sh. milioni 11.6, huku ujenzi ukiendelea.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# Tuwaunge mkono wachezaji Taifa Stars wataweza AFCON

**TAIFA** Stars imeelekea Misri kwa kambia ya wiki moja kabla ya safari ya Ivory Coast Januari 8, mwaka huu tayari kwenda kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye fainali za Mataifa ya Afrika zitakazofanyika nchini humo kuanzia Januari 13, mwaka huu.

Fainali hizo ambazo Tanzania ni mara ya tatu kushiriki katika historia ya michuano hiyo, itaanza kutupa karata yake ya kwanza Januari 17 dhidi ya Morocco, kwenye Kundi lao la E, pia zimo DR Congo na Zambia.

Kuelekea fainali hizo Kocha Mkuu wa Stars, Adel Amrouche amepewa uwanja mpana kuchagua wachezaji 25 kutoka 53 aliowaita katika kikosi cha maandalizi awali atakaoenda nao Ivory Coast.

Ni wazi katika uchaguzi huo wa Amrouche, hauwezi kumrithisha kila mtu, wapo baadhi watakosoa na wengine hadi kushangazwa kwa baadhi ya wachezaji ambao walitamani kuwaona katika fainali hizo kubwa zaidi barani Afrika.

Lakini ifahamike kwamba kote duniani, hakuna kocha wa timu ya taifa ambaye huita kikosi chake na kuungwa mkono na mashabiki ama na raia wote, hivyo Amrouche anaweza kukosolewa lakini tunatamani kuona kuwe kwa kujenga na si kubomoa.

Hii ikiwa na maana tunapaswa kuwasapoti wachezaji waliopata nafasi hiyo kwa kila kitu ili kuwatia moyo na kujiona mashujaa wanapoelekea kuipeperusha bendera ya Tanzania katika fainali hizo.

Kwa mashabiki, wachambuzi wa soka na wanahabari kwa ujumla, wanapaswa kutambua kwamba kila wanachokizungumza kinawafikia wachezaji, hivyo hawana budi kuwazungumzia katika hali ya uchanya zaidi ili kuwatia moyo badala ya kuongeza maneno hasi zaidi jambo ambalo litawafanya kwenda kupambana kinyonge.

Nipashe tunaamini hata kama Stars haitafanya vizuri katika fainali hizo sababu haiwezi kuwa ni kuachwa kwa mchezaji fulani bali itakuwa tu imezidiwa kimbinu na wapinzani wao.

Sisi tukiwa wadau wakubwa wa michezo nchini, tunaamini katika kucheza kitimu, ingawa pia uwezo binafsi wa mchezaji mmoja mmoja katika kikosi ni muhimu, lakini viwango vya wachezaji wetu havitofautiani sana, hivyo walioitwa watakwenda kulipambania taifa vema katika michuano hiyo.

Kikubwa ni katika tathmini ya kikosi cha Amrouche, kutoa kauli nzuri za zitakazosaidia kuwajenga kisaikolojia na kwa kuwaaminisha wanaweza kupambana na timu yoyote na kupata matokeo chanya, lakini Watanzania wote wakiungana kuwa nyuma yao kwa kuwasapoti badala ya kuanza kunyooshea vidole baadhi ya wachezaji kuwa hawakustahili kujumuishwa.

Ikumbukwe pia Taifa Stars inakwenda kukutana na timu ngumu na zenye uzoefu mkubwa katika michuano hiyo huku wachezaji wao wengi wakitoka kucheza katika ligi kubwa Ulaya, hivyo huu ni wakati kwao waanza kuzoea mikikimikiki hiyo.

Hivyo matokeo yoyote itakayopata Taifa Stars hususan mchezo wao wa kwanza dhidi ya timu ngumu na zoefu ya Morocco, tunapaswa kuwatia moyo wa kijasiri ili kupambana zaidi.

Katika hilo, ni wakati pia kwa wenye uwezo kuungana timu hiyo kwenda kuipa sapoti kwani mara nyingi hilo pia huikwamisha Taifa Stars kwa kukosa mchezaji wa 12 uwanjani ambaye ni mashabiki tofauti na nchi za wenzetu ambazo hujazana viwanjani kuishangilia timu yao.

Tunatambua kutokana na hali ngumu kiuchumi ni vigumu kwa mashabiki kutoka nchini kwenda Ivory Coast, hivyo katika kipindi hiki sote hatuna budi kuisapoti kupitia mitandao ya kijamii, vyombo vya habari na hata kwa simu badala ya kuwakosoa na kutoa maneno ya kuwakatisha tamaa mashujaa wetu tuliowatuma kupambania nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Tusiwatishe, kuwabeza wazawa wanaotakiwa na Simba, Yanga

**NI** kipindi cha usajili wa dirisha dogo lililofunguliwa Desemba 16, mwaka jana huku likitarajiwa kufungwa Januari 16, mwaka huu ambapo kwa mujibu wa Bodi ya Ligi ni kwamba kutakuwa na uhamisho wa wachezaji kwa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, Ligi Daraja la Pili 'First League' na Ligi Kuu Soka Wanawake.

Timu zipo kwenye harakati za kuongeza wachezaji ambao wanaona watawafaa kwenye ngwe iliyobaki, kwani ukiangalia kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Championship, ni kama vile tayari timu nyingi zimeshamaliza mzunguko wa kwanza.

Klabu za Simba na Yanga zinasaka wachezaji ambao mbali na ligi, lakini watakaokuja kuwaongezea nguvu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Pamoja na kuwa mahitaji makubwa ya timu hizi ni kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi, lakini zimeonekana kutaka pia wachezaji wa Kitanzania.

Yanga imeshamsajili mchezaji, Shekhan Ibrahim Hamisi kutoka JKU ya Zanzibar, wakati Simba ikiwa kwenye hatua za mwisho za kumsajili Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar.

Mbali na huyo, Simba pia inatajwa kuwa katika harakati za kuwasajili wachezaji wengine wazawa, nao ni mchezaji anayecheza nafasi ya straika na winga kutoka Prisons, Edwin Barua, pamoja na straika anayekuja juu kwa sasa, Valentino Mashaka wa Geita Gold.

Imejengwa kasumba hapa nchini kwa baadhi ya mashabiki na wachambuzi kutokuwa na wasiwasi wanaposikia klabu kubwa haswa za Simba na Yanga zinataka kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi.

Wanakuwa na wasiwasi, pamoja na maneno mengi ya kejeli na kuwatisha wanaposikia wachezaji wazawa wanasajiliwa.

Tumeona hata klabu inapomtangaza mchezaji mzawa, mashabiki wamekuwa hawafurahii na wengine kuongea maneno yanayoashiria kuwa viongozi hao hawapo makini.

Wachambuzi nao wanawabeza, lakini wanakwenda mbali zaidi na kuwatisha kuwa klabu hizo ndizo kaburi la wachezaji hao.

Maana yake ni kwamba wanakwenda kuua vipaji vyao. Imefika wakati mpaka washauri wa wachezaji wao wanawakataza kwenda Simba au Yanga kwa kile walichoaminishwa kuwa hawawezi kucheza, badala yake viwango vyao vitashuka.

Binafsi, napinga hili, na kama kuna mchezaji yeyote wa Kitanzania anatakiwa na Simba au Yanga asiogope, aende na atacheza soka.

Hakuna mchezaji yeyote wa Kitanzania ambaye amezaliwa kwenye hizo timu, wote wametoka walikotoka na wanang'ara kwa sababu wanafanya tu kile ambacho kimewapeleka pale.

Mohamed Husssein 'Tshabalala' ametoka Kagera Sugar, Shomari Kapombe, ametokea Polisi Morogoro, baadaye Azam FC na kurejea Simba, John Bocco, ametokea Azam FC, Kibu Denis alitokea Mbeya City, Mzamiru Yassin yeye awali alikuwa Mtibwa Sugar, Kennedy Juma, Singida United.

Hawa wote wanacheza Simba na wanawika, kwa sababu wameamua kuwa mpira ndiyo kazi yao na ndiyo maisha yao.

Aboubakar Salum ametokea Azam FC, Mudathir Yahaya ndiyo kabisa yeye alikuwa hana hata timu, Dickson Job, Kibwana Shomari wote wametokea Mtibwa Sugar, Bakari Mwamnyeto Coastal Union, Clement Mzize amepandishwa kutoka kikosi cha pili.

Hawa ni wachezaji wa Kitanzania wanaoing'arisha Yanga, wangeogopa kujiunga na timu hiyo wangekuwa hapo walipo?

Mimi nafikiri wanaoshindwa 'maisha' kwenye klabu hizo ni wale ambao hawakujiandaa kiakili na kimwili, au kujiandaa na maisha ya ustaa.

Unaposajiliwa tu Klabu ya Simba au Yanga, kabla hujacheza tayari unakuwa staa, hapo unatakiwa sasa kuuliza ustaa huo kwa pesa unazozipata, marafiki, na hata aina ya maisha mapya, pamoja na kutenga muda wa mazoezi.

Hilo ndilo linalowashinda wachezaji wengi wa Kitanzania wanaojiunga na klabu hizi na kulalamika vitu vingi visivyo vya msingi kuwa klabu zinaua vipaji vya wazawa.

Unashangaa mbona havijaua vipaji vya akina Job na Kapombe waliocheza miaka nenda rudi?

Nawashauri wachezaji wote wazawa, yoyote anayepata dili kusajiliwa na Simba au Yanga achangamkie fursa haraka, asiogope kwenda, kinachotakiwa ni kuacha mambo mengi akili iwe kwenye soka.

Nina uhakika watawavua watu namba. Hakuna aliyetegemea kuwa winga Ulimboka Mwakingwe aliyesajiliwa kutoka timu ya Reli ya Morogoro iliyoshuka daraja miaka ya nyuma, angemvua namba staa wa Simba wakati huo, Stephen Mapunda 'Garincha.'

HABARI KITAIFA

# Wastaafu wamwangukia Rais Samia malipo kiduchu pensheni

**Na Grace Gurisha**

UMOJA wa Jamii ya Watanzania Waliostaafu Kazi (UJAWATA), wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwaongezea pensheni ya kima cha chini kutoka Sh. 100,000 waliyolipwa sasa hadi Sh. 500,000.

Wamesema kwa sasa hali ya maisha imepanda, wakiongezewa itawasaidia katika matibabu kutokana na wengi kusumbuliwa na magonjwa ya uzeeni.

Mwenyekiti wa umoja huo, Sadiki Msuya, alitoa ombi hilo jana kwa niaba ya wastaafu wenzake wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

"Hawa ni wastaafu waliofanya kazi serikalini, dhumuni letu kubwa na kilio chetu ni pensheni tunaliyolipwa na mfuko wa PSSF sawa kima cha chini cha Sh. 100,000 kwa hali halisi ya maisha ya leo ni kiwango kidogo sana hakikidhi maisha," alisema.

"Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan atuongezee angalau kima cha chini kianzie Sh. 500,000. Tunajua serikali ina mambo mengi na ina kazi nyingi za kufanya, lakini ituangalie kwa sababu na sisi tuliitumikia nchi hii, tukaijenga ikafika hapa ilipofika tukapumzika tukawaachia kijiti wengine," alisema Msuya.

Alisema suala hilo wamelifutilia kwa muda mrefu bila mafanikio ndio maana wakaamua kutumia vyombo vya habari kufikisha kilio chao kwa Rais Samia kwasababu wanaamini hafahamu kuna wastaafu wanalipwa kiwango hicho.

Katibu wa UJAWATA, Profesa Haizer Laizer aliomba mamlaka husika kuliangalia suala hilo kuwezesha kuboresha maisha ya wastaafu ili na wao waishi maisha stahiki yenye staha.

"Kama suala ni sheria basi vifungu vya sheria za PSSF vibadilishwe kwa sababu vimepitwa na wakati kwa sababu kila siku maisha yanabadilika. Tunaomba Rais asikie kilio chetu kwa kuwaongezea pensheni yetu," alisema Profesa Laizer.

Mmoja wa waastafu hao, Grace Msangi alisema wana hali mbaya ya maisha kwenye suala la afya, wengi wanatumia dawa kali kutokana na kusumbuliwa na magonjwa, pia lishe kwao ni ngumu na wanashindia chai na maandazi mawili.

"Mama tunaomba usikie kilio chetu wewe ni malikia wetu wa nguvu huna baya na mtu, tunaomba uione hili tatizo kwetu kwa sababu hali ni mbaya. Wazee wanakunywa dawa kali sana, lishe hawana hali inayosababisha magonjwa mengine yazalishwe," alilalamika.

**Mwenyekiti wa umoja huo, Sadiki Msuya, alitoa ombi hilo jana kwa niaba ya wastaafu wenzake wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.**



Katibu Mkuu wa Taasisi ya Umoja wa Amani Kwanza inayojishughulisha na utoaji wa elimu ya amani, Netho Ndilito, akizungumza katika ziara ya Mkoa wa Dar es Salaam jana kwa ajili ya kuzungumza na wanataasisi kuhusu kuimarisha taasisi hiyo. Katikati ni Rais wa Taasisi hiyo, Dk. Wilson Mgunza na kulia ni Makamu wa Rais wa Taaisisi, Alex Mnyangambe. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Biteko awapongeza walimu kuongeza ufaulu shuleni

**Na Mwandishi Wetu,**
GEITA

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko amewashukuru walimu wanaofundisha shule za msingi na sekondari wilayani Bukombe kwa kuwajali na kuwafundisha wanafunzi kwa weledi na maarifa, hali iliyosababisha wilaya hiyo kuwa na ufaulu mzuri.

Dk. Biteko ambaye ni Mbunge wa Bukombe, alitoa pongezi hizo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kabuhima, Kata ya Uyovu wilayani Bukombe mkoani Geita ikiwa ni sehemu ya ziara zake.

"Nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru walimu wote katika Wilaya ya Bukombe, wametupa heshima kubwa miaka ya nyuma ambayo ni 2015 kurudi nyuma, hata tulipokuwa tukipangwa kimkoa katika matokeo ya darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita tulikuwa katika nafasi ya mwisho," alisema na kuongeza:

"Lakini leo walimu wa wilaya yetu wamefanya kazi kubwa, wametuheshimisha kwani katika Mkoa wa Geita kama hatuwi wa kwanza, basi tunakuwa wa pili."

Alisema ufaulu huo mzuri unatokana na walimu hao kuwajali, kuwafundisha wanafunzi vizuri unawawezesha wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao.

Aidha, alikemea tabia ya baadhi ya wazazi na walezi kutopeleka watoto shule kwa nia ya kuwaozesha na kupata mahari, akisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amejenga shule nyingi nchini, wajibu wa wazazi ni kupeleka watoto shule na sio kuwakwamisha.

Dk. Biteko ambaye ni Waziri wa Nishati, alisema miradi mbalimbali ya maendeleo inaendelea kutekelezwa ikiwamo ujenzi wa shule za msingi na sekondari, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na ujenzi wa taa za barabarani utakaoanza Januari, mwakani.

Katika hatua nyingine, Dk. Biteko alizindua wodi mpya katika Hospitali ya Kumbukumbu ya Charles Kulwa iliyoko Runzewe wilayani Bukombe na wodi hiyo ni maalum kwa ajili ya kuhudumia wajawazito wanaofanyiwa upasuaji.

Akiwa hospitalini hapo, Dk. Biteko alipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya hospitali hiyo iliyoanzishwa mwaka 1992 ikiwa kama zahanati.

Mwaka 2005 ilipanda hadhi ya kuwa kituo cha afya na mwaka 2020 ilipandishwa hadhi ya kuwa hospitali ya wilaya, aliupongeza uongozi wa hospitali hiyo inayohudumia wagonjwa takribani 72,000 kwa mwaka.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella ambaye alikuwa mgeni maalum, alimshukuru Rais Samia kwa kazi nzuri anayoifanya kuinua sekta afya katika Mkoa wa Geita na maeneo mengine nchini.

Aliwataka wadau wengine kuiga mfano wa wamiliki wa hospitali hiyo kwa kuhudumia wagonjwa wengi na kutoa huduma kwa kiwango cha hali ya juu hadi kufikia hatua ya kupandishwa hadhi.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Ubovu barabara wakwamisha usafirishaji wa madini

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imeombwa kutengeneza miundombinu ya Barabara ya Ruangwa Mjini kwenda Kata ya Matambale ulipo mgodi wa uchimbaji madini ya Kinywe.

Lengo la ukarabati wa barabara hiyo ni kuwezesha magari yatakayobeba mzigo huo kupeleka sokoni bila tatizo.

Ombi hilo limetolewa na Meneja wa Kampuni ya Lindi Jumbo Ltd., Chediel Mshana, alipokuwa anatoa taarifa kwa Waziri wa Madini, Antony Mavunde, aliyetembelea mgodi huo.

Akiwasilisha taarifa kwa Waziri Mavunde alisema, urefu wa barabara hiyo kutoka Ruangwa Mjini hadi eneo ulipo mgodi ni kilomita 36, inahitaji kujengwa madaraja makubwa mawili na kuongeza upana.

Alisema ujenzi wa mgodi huo umekamilika kwa asilimia 90 na unatarajia kuanza kazi Machi mwakani, huku akitaja matatizo yanayokutana nayo ni upatikanaji wa umeme.

Alitaja tatizo lingine ni kucheleweshwa kupatiwa kwa wakati mizigo Bandari ya Dar es Salaam inayoagizwa kutoka nje ya nchi na benki kuchelewa kuipa kampuni hiyo fedha za mkopo zinayotoka nje ya nchi.

"Mitambo na vifaa vingine inatoka China inapofika bandarini inachukua muda mrefu kutolewa, alisema Mshana.

Alisema mgodi huo ni wa tatu duniani na unathamani ya Dola za Marekani milioni 33.0 (Sh. bilioni 75) huku ukiwa na wafanyakazi 275 wakiwamo vibarua, kati yao 75 ni vijana kutoka vijiji vinavyouzunguka mgodi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassani Ngoma, alisema kuwapo kwa mgodi huo kutapunguza tatizo la ajira kwa vijana wa maeneo ya vijiji husika.

Alimwomba Waziri Mavunde kukutana na waziri mwenzake wa nishati kuharakisha upelekaji huduma ya umeme kwenye mgodi huo ili uweze kufanya kazi ya uzalishaji.

Akizungumza na watumishi wa kampuni hiyo, Waziri Mavunde alisema serikali ipo tayari kushughulikia matatizo yanayouakwamisha mgodi huo.

Alisema uzalishaji utakapoanza taifa litanufaika kupata mapato yake kupitia tozo, ushuru, kodi na kiasi kingine kurejeshwa kwa jamii inayowazunguka mgodi husika kupitia mauzo yanayotokana na madini pale utakapoanza kufanya kazi ya uzalishaji wake.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kulia) ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Bukombe, akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella, wakizindua wodi mpya katika Hospitali ya Kumbukumbu ya Charles Kulwa, iliyopo Runzewe wilayani Bukombe, Mkoa wa Geita. **PICHA: THERESIA MHAGAMA**

## Wenye leseni 'bubu' uchimbaji madini kunyang'anywa

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WAZIRI wa Madini, Anthony Mvunde amewataka wafanyabiashara waliopewa leseni za kufanya utafiti wa madini mkoani Lindi kuzifanyia kazi, vinginevyo watachukuliwa sheria kali ikiwamo kuwanyang'anya umiliki.

Alitoa taarifa hiyo juzi mkoani hapa wakati akizungumza na wafanyakazi wa Kampuni ya Lindi Jumbo Ltd inayohusika na uchimbaji na uchakataji madini ya Kinywe, wilayani Ruangwa.

Waziri Mavunde alisema serikali inasimamia miradi mbalimbali mikubwa inayohitaji kuwekezwa maeneo ya madini ya kimkakati nchini kwa lengo la kuongeza mapato na ajira kwa wananchi.

Alisema Mkoa wa Lindi pekee una leseni za utafiti 112, lakini taarifa zilizopo zinazofanyakazi zipo chache bila kutaja idadi yake.

"Wale wote walio na leseni za utafiti, lakini hawazifanyii kazi watanyang'anywa na kupewa watu wengine walio na uwezo," alisema Waziri Mavunde.

Kadhalika, alisema kwa mujibu wa sheria wafanyabiashara waliopewa leseni na hawazifanyii watapelekewa notisi ya kuwajulisha lengo la kuwanyang'anya na kuwapa wawekezaji walio na uhitaji kufanya hivyo.

Mavunde alisema: "Kila eneo unalogusa lina mtu, lakini uoni kazi inayofanyika. Sasa tunakwenda kuwanyang'anya watu ambao hawaendelezi maeneo yao."

Alisema lengo la serikali ni kuona shughuli za madini zinafanyika katika eneo kubwa ndani ya nchi ili yaweze kutoa mchango mkubwa kwa pato la taifa na kueleza Mkoa wa Lindi pekee umepangiwa kukusanya Sh. bilioni 6.2 kutoka katika kodi za madini.

Waziri Mavunde yupo mkoani Lindi ikiwa ni ziara ya siku moja, lengo kuu likiwa ni kuona kazi za ujenzi wa mgodi wa madini aina ya Kinywe unaojengwa katika Kata ya Matambalale, Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi.

## Familia ya waziri wa zamani yalia na uzushi mitandaoni

**Na Gwamaka Alipipi**

FAMILIA ya aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, marehemu Abdalla Saidi Natepe, wamesikitishwa na taarifa za uzushi zinazozunguka katika mitandao ya kijamii zikieleza kwamba baba yao alimfukuza kwa nguvu Rais mstaafu, Ali Hassan Mwinyi kwenye nyumba ya serikali alipomrithi katika nafasi hiyo mwaka 1980.

Natepe alimrithi Rais mstaafu Mwinyi kwenye wizara hiyo na baadaye aliteuliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza na Nipashe, msemaji wa familia ya marehemu Natepe, Ismail Said alisema kwamba wamesikitishwa na taarifa hizo ambazo familia haifahamu nia yake ni nini, akisema kwamba ni za kupotosha hutoka kila inapokaribia uchaguzi mkuu.

"Baba yetu alikuwa ni Waziri wa Mambo ya Ndani wakati Hayati Julius Nyerere akiwa Rais. Tumezaliwa na kukulia Upanga jijini Dar es Salaam tangu mwaka 1977. Mpaka sasa tunaishi Upanga na hatujawahi kuishi Oysterbay ambako kuna hiyo nyumba ambayo Mwinyi aliishi."

Alisema taarifa hizo zinachapishwa ili kuharibu taswira ya familia na kuwaonya wote walionyuma ya taarifa hizo na kuzisambaza kuacha kabla sheria haijachukua mkoando wake.

Alisema kwa sasa familia inafanya kazi na vyombo vya dola ikiwamo Jeshi la Polisi kuwasaka watu wanaosambaza taarifa hizo ambazo zinaleta chuki kati ya watu na watu.

Kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Rais mstaafu Mwinyi alihudumu kama waziri katika wizara hiyo mwaka 1975 hadi 1976 wakati Natepe (marehemu) alihudumu kuanzia mwaka 1980 hadi 1983.

Kadhalika katika kitabu chake cha safari ya maisha yangu, Rais Mwinyi ameandika kwamba aliishi Oysterbay kabla ya kufanyika kwa mabadiliko ya Baraza la Mawaziri mwaka 1976 na alihamishiwa kwenda Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kwenye kitabu hicho, Rais mstaafu Mwinyi anasema baadaye alihamishiwa kwenda wizara inayoshughulikia Muungano, hatua hiyo ilimlazimu ahamie Zanzibar kwa sababu makao makuu ya wizara yalikuwa huko na kuiacha nyumba aliyokuwa anaishi maeneo ya Oysterbay waziri mpya aliyechukua nafasi yake, kwa wakati huo alikuwa ni Jackson Makweta.



## Makatibu muhtasi wawakumbuka waathirika Hanang'

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAKATIBU muhtasi wa wizara mbalimbali na taasisi za umma kutoka Mkoa wa Dodoma, wamepeleka misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa maporomoko ya tope, mawe na magogo yaliyotoka Mlima Hanang', yakiwamo mahitaji ya wanafunzi.

Misaada hiyo, ambayo ni vifaa vya shule na mahitaji mengine muhimu, vina thamani ya Sh. milioni tano.

Akikabidhi misada hiyo mwishoni mwa wiki, Mwakilishi wa Chama cha Makatibu Muhtasi mkoani humo (TAPSEA), Conjeta Chambila, alisema baada ya kushuhudiwa kwa maafa hayo, waliguswa na kuamua kuanza kuchangishana ili kuwashika mkono waathirika wa maafa hayo.

Aliikabidhi misaada hiyo kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara, Athmani Likeyekeye.

Alisema misada hiyo inalenga kuwapiga jeki wanafunzi na wanawake kupata mahitaji ya shule na ya nyumbani ili wasiweze kushindwa kuhudhuria masomo na wanawake kuendelea na shughuli zao.

"Baada ya kuona maafa ya maporomoko ya tope, mawe na magogo tulijikusanya na kutafuta namna ya kuja kuwashika mkono wenzetu wa Hanang'," alisema Chambila.

Akizungumzia misaada hiyo Katibu Muhtasi kutoka Wizara ya Ujenzi, Devotha Mbuya alisema, waliamua kuja kutoa pole kwa waNaHanang' kwa shida iliyowakuta.

"Tulikusanya nguo, viatu na mabegi kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya wanafunzi na wanawake ili wakapate sare wasome na wanawake waendelee na shughuli zao," alisema Mbuya.

Aidha, alisema vitu vingine walivyowaletea ni madaftari, kalamu, majola matano ya vitambaa vya kushona sare na mahitaji mengine ya shule.

Naye Katibu Muhtasi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Habiba Mhina, alisema waliguswa na wenzao waliopata maafa wakaona ni vizuri wawaletee sare za shule wanafunzi.

Mhina, alisema licha ya kutokea maafa maisha lazima yaendelee hivyo wamewaletea mahitaji watoto wote bila kujali jinsia.

Pia walitembelea maeneo yaliyoathirika na maafa ikiwamo Kata ya Gendabi, Ganana na Jorodom ili kujionea maafa yalivyoathiri wananchi.

Katibu Tawala wa Wilaya, Likeyekeye, aliwashukuru kwa kitendo walichokifanya kuwa ni cha kizalendo na chenye utu.

Likeyekeye, alisema kwa kutoa misaada hiyo wamemuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye ndio alitangulia kutoa pole kwa waathirika na kutoa maelekezo ya namna ya kuwasaidia.

Mmoja wa waathirika wa maafa kutoka Kijiji cha Gendabi, Daud Masaay, alisema serikali na wadau wanaotoa misaada ya kibinadamu inawapa nguvu ya kuanza maisha mapya baada ya kupoteza mali zao na ndugu zao.

# Hatima vijiji vitatu vya hifadhi mikononi mwa serikali

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

HATIMA ya wananchi wa vijiji vitatu vya Kata ya Ilorienito, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, waliovamia Msitu wa Hifadhi wa Mlima Ketumbeine, sasa iko mikononi mwa serikali, baada ya ilani ya kuwataka kuondoka kwa lazima kufikia ukomo wake Desemba 31, mwaka jana.

Mwanzoni mwa mwezi Desemba 2023, Mkuu wa Wilaya, Marko Ng'umbi, alitoa nyongeza ya siku 18 ya kuwataka wananchi wa vijiji vya Nadare, Losirwa na Ilorienito waliovamia msitu huo kuondoka kwa hiari, badala ya kusubiri matumizi ya nguvu.

Wananchi hao ambao ni wafugaji jamii ya Kimasai, wanadaiwa kuharibu vyanzo vya maji na kuhujumu shughuli za uhifadhi wa msitu huo kwa kuendesha shughuli za kilimo, kujenga makazi, kukata miti ovyo na kuchungia mifugo ndani ya vyanzo vya maji.

Wakati amri hiyo ya kuondoka ikiwa imefikia ukingoni, Shirika la Kimataifa la World Wide Fund (WWF), limelazimika kuendelea na kampeni ya kurejesha uoto wa asili katika msitu huo wa hifadhi kwa kupanda miti.

"Niliwapa miezi mitatu, maboma yote yaondoke. Tulikubaliana hivyo pale Kijijini Losirwa kwenye mkutano, pale Ilorienito na Nadale; tukakubaliana hivyo pale Njoro, kule Sokoni na tukakubaliana hivyo kwenye mkutano pale Langa'ta Dabashi.

"Nilisema ondokeni kwa hiari yenu na ndio maana mmepewa muda wa kujiandaa kuondoka mrudi upande wa pili. Huko mnakorudi ni huruma ya serikali.

"Ukweli ni kwamba hali ya msitu wetu ni mbaya. Ni mbaya kwa sababu watu wamevamia kwenye vyanzo vya maji, watu wameingia kulima msituni. Ni mbaya kwa sababu watu wanakata miti, watu wameanzisha makazi, ni mbaya sana kwa sababu watu wanaingiza mifugo mpaka juu kabisa viliko vyanzo vya maji."

Meneja wa Mradi Land for Life, Reguli Marandu, akizungumzia kampeni hiyo alisema:

"Tumekuwa tukifanya kazi za uhifadhi katika vijiji vyenu na tukisema uhifadhi tunaangalia uhifadhi wa mazingira, tunaangalia uhifadhi wa wanyamapori lakini tunaangalia namna gani uhifadhi unasaidia jamii zile zinazozunguka hayo mazingira, ambayo tunayahifadhi.

"Dhana ya WWF, tunataka jamii zile zinazoishi kwenye hayo mazingira pamoja na wanyamapori na mazingira yetu, vyote viwe vina ustawi ambao ni mzuri.

"Tunawajibu kama wakazi wa kata hii tunatunza msitu ambao unazunguka vyanzo vya maji. Tumewawezesha kufanya kilimo cha alizeti, mkikosa maji mtalima alizeti? Haya yote ni kwa ajili ya kuwawezesha kuongeza kipato.

"Ni jukumu letu sisi ambao tunakaa karibu na vyanzo vya maji, tuwe sehemu ya uhifadhi na ukimuona mtu anakata miti unatakiwa utoe taarifa kwenye kamati ya ulinzi ya kijiji chenu. Namwahidi Mkuu wa wilaya kwamba tutaongeza, tutaleta miti mingine tena kama 500."

Diwani wa Kata ya Ilorienito, Sano Otusu, aliwahadharisha wakazi wa vijiji hivyo kuwa, hakuwaomba kura ili aje awaruhusu kwenda kuishi ndani ya misitu.

Otusu alifafanua, "Naomba niwaambie ukweli, msitu ni msitu na maeneo ya kilimo ni ya kilimo, mkae mkijua hilo kwamba serikali ina dhamira njema sana kupanda miti ili kuokoa misitu yetu isije ikatoweka.

"Sikuwaomba kura ili niwaruhusu kwenda kuishi ndani ya misitu, nilisema nakwenda kuwasaidia kuleta miradi na ndio mradi ambao naupambania kisiasa, maji yapo, umeme, barabara na kadhalika."

Msitu wa Hifadhi wa Ketumbeine, ulitangazwa kuwa eneo la msitu wa hifadhi ya Mlima Ketumbeine mwaka 1958.



Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki (katikati), akizindua uvunaji wa mazao ya viungo kwenye shamba la pilipili manga la Mkulima Hamisi Machupa, jana katika Kijiji cha Bombani. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina na kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Dk. Jumaa Mhina. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Watalii raia wa China wapanda milima mirefu duniani watua nchini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KUNDI la watalii 54 maarufu wa kupanda milima mirefu duniani kutoka China, limewasili nchini kwa ajili ya kushiriki tamasha la kupanda Mlima Kilimanjaro.

Kundi hilo liliwasili mkoani hapa mwishoni mwa wiki na kupokewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela na walifanya mazungumzo na kushiriki chakula cha jioni.

Watalii hao 54 wakiongozwa na Xia Boyu, wako nchini kwa ajili ya kushiriki tamasha la kupanda Mlima Kilimanjaro, lililoandaliwa na kampuni ya kitanzania ya Gosheni Safaris.Akizungumza wakati wa hafla ya kuwapokea watalii hao, Mongela alisema, ujio wa wageni hao umetokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na China, ambao ulitengenezwa na waasisi wa mataifa hayo na kuendelezwa na viongozi walioko sasa.

"Nichukue fursa hii kuwakaribisha Tanzania, kushiriki Tamasha la Kupanda Mlima Kilimanjaro, ukiwa ndio msimu mzuri wa kupanda Mlima Kilimanjaro, ninaamini mtafurahia mwonekano na mandhari nzuri ya mlima huo mrefu Afrika," alisema Mongella.

Pia ameipongeza Kampuni ya Utalii ya Goshen safaris kwa kundaa tamasha hilo, ambalo ni muhimu na lenye manufaa kwa Tanzania na nchi nyingine duniani ikiwamo China.

Alisema msimu wa mwisho wa mwaka, ni mzuri zaidi kwa kupanda mlima huo kwa kuwa mandhari iliyoko kwa sasa itawafanya kufurahia vizuri na kuitangaza Tanzania kupitia Mlima Kilimanjaro.

Licha ya kuwakaribisha katika hafla hiyo, Mongella aliwapatia vyeti vya kuwapongeza wapanda mlima hao maarufu dunia, ambao wamekwishapanda mara 10 Mlima Evarest ambo ni mrefu zaidi duniani.

Naye Kiongozi wa watalii hao, Boyu amefurahishwa kuwapo Tanzania na kuvutiwa na mandhari nzuri ya Mkoa wa Arusha, huku akiamini safari yao ya siku 10 itakuwa nzuri na ya furaha kwa wote.

"Tumefurahi kuwa Tanzania, kwa kuwa ni nchi nzuri, pia watu wake ni wazuri wana upendo, safari yetu itakuwa nzuri na ya furaha, tunafurahia kupanda Mlima Kilimanjaro, lakini tunafurahi zaidi kushiriki tamasha hili kubwa," alisema Boyu.

Wageni hao watakuwa nchini kwa siku 10, wakitumia siku saba kupanda Mlima Kilimanjaro na siku tatu kwa ajili ya safari.

Ujio wa watalii hao ni matokea ya Filamu ya Royal Tour, iliyochezwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ukiwa ni mkakati wa kutangaza utalii ndani na nje ya nchi.



# Mwananchi ajitolea nyumba kuwa kituo polisi Ukerewe

**Na Thomas Wandiba,** SAUT

MKAZI wa Kata ya Ilangala, Kisiwa cha Gana, wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza amejitolea nyumba yake aliyokuwa anaitumia na kuikabidhi kwa Jeshi la Polisi ili iwe Kituo cha Polisi kwa ajili ya kutoa huduma za usalama kwa wakazi zaidi ya 6,000 wa kisiwani humo.

Nyumba hiyo yenye vyumba zaidi ya 15 inatakiwa kufanyiwa ukarabati mdogo wa kuwekewa miundombinu na mifumo ya majitaka itakayokidhi hadhi ya kituo cha polisi.

Akizungumza juzi na wananchi wa kisiwa hicho, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Wilbrod Mutafungwa, alisema kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha polisi utatatua kero za kiusalama ambazo zinawakabili kisiwani hapo.

"Niwapongeze wananchi wa eneo hili kwa kukubali kujenga kituo cha polisi katika eneo hili, ikiwezekana kabla ya mwishoni mwa mwezi Januari 2024 pengine kituo hicho kiwe kimekamilika na mimi nitatamani sana kuja kukizindua ili tuweke askari wa kutosha kuanza kufanya kazi," alisema Mutafungwa.

Wakazi wa kisiwa hicho walitaja eneo hilo kukithiri kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili, ulevi, utovu wa nidhamu, wizi wa nyavu na injini za mitumbwi, uvuvi haramu, ukatili wa kijinsia, udokozi, mauaji, unyanyasaji na ukosefu wa alama za mipaka ziwani zinazoonyesha mpaka wa Tanzania na Uganda.

"Tunaomba Jeshi la Polisi lihakikishe linadhibiti vitendo hivi kwa kufanya ukaguzi na doria za mara kwa mara hususani katika maeneo ya mipaka ya Tanzania na Uganda ili tuwe na amani na usalama," alisema Swai Somba, mvuvi wa kisiwani hapo.

Akijibu suala la mipaka, Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri na Uvuvi endelevu Ziwa Victoria, Bakari Kadabi alisema, kuanzia Januari 2024 serikali inatarajia kuweka mipaka ziwani itakayokuwa inawasaidia wavuvi kujua upande wa Tanzania na Uganda.

Vilevile, Kamanda Mutafungwa alitangaza operesheni kabambe na endelevu ndani ya Ziwa Victoria na maeneo mengine ili kutokomeza uhalifu na kuimarisha ulinzi na usalama zaidi katika maeneo yote.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Kitengo cha Polisi Jamii Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Salige, aliwataka wananchi wa Kata ya Buzuruga, wilayani Ilemela kuanzisha vikundi vya polisi jamii ili kushirikiana na polisi katika kuimarisha ulinzi katika maeneo yao.

Wananchi hao wanadaiwa kugomea mchango wa Sh. 2,000 kwa ajili ya vijana wanaofanya kazi hiyo nyakati za usiku wakidai kuwa fedha hizo haziwafikii walengwa hali inayosababisha vitendo vya uvunjifu wa amani kukithiri katika kata hiyo.

Aidha, polisi kata wa eneo hilo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Gerard Mafyuguru aliwahakikishia wananchi kuwa programu ya ulinzi shirikishi inarudi na kuwataka kushiriki kikamilifu ili kudhibiti uhalifu.




Meneja Mwandamizi wa Bima za Mali NMB, Adam Nsenga, akizungumza kwenye hafla ya ulipaji fidia kwa wamachinga 15 wa soko la Mlango Mmoja jijini Mwanza, walioathiriwa biashara zao na mvua. Kushoto ni Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Hamadan Silliah na Ofisa Ubora wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khalfan Isango.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Burian aonya wanaohujumu miundombinu barabara

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burian, amewaonya watu wanaojihusisha na vitendo vya wizi na uharibifu wa miundombinu ya barabara na kuahidi kuwachukulia hatua kali ikiwamo kuwafikisha mahamani kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki katika ziara ya siku moja Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, kukagua ujenzi wa barabaa ya Kazilambwa-Chagu yenye urefu wa kilomita 43 inayojengwa kwa kiwango cha lami.

Alisema wapo baadhi ya watu au kikundi cha watu ambao kazi yao ni kuiba, kugonga na kuharibu miundombinu ya barabara na kuwa serikali haitowavumilia kwa kuwanasa na kuwafungulia kesi za uhujumu uchumi.

Balozi Dk. Burian aliuagiza Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) mkoani Tabora, kuhakikisha barabara hiyo ya Kazilambwa-Chagu yenye urefu wa kilomita 43 inawekewa taa za barabara kwa maeneo sahihi zinapopaswa kuwekwa na kwa wakati uliopangwa.

Katika hatua nyingine wakati akiongea na wananchi, aliwataka wanawafichua wanaohusika na hujuma hizo ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Meneja TANROADS Mkoa wa Tabora, Mhandisi Raphael Mlimaji, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kuchukua hatua kali ikiwamo kuwafikisha mahakamani na wengine kulipa faini watakapobainika kuharibu miundombinu hiyo.

Alisema jukumu la kulinda miundombinu ya barabara ni la kila Mtanzania na kwamba lazima jamii itambue kuwa serikali inatumia fedha nyingi kwenye kutekeleza miradi yake.

Aliahidi kutekeleza maagizo yote ya Mkuu huyo ikiwa ni pamoja na uwekaji wa taa za barabarani ambazo zipo tayari katika Barabara ya Kazilambwa-Chagu.

Mkazi wa eneo hilo, Juma Fadhiri, alimhakikishia mkuu huyo kuwa watajitahidi kufanya ulinzi katika eneo hilo na kama watawakamata watu wanafanya hivyo watawafikisha kwenye vyombo vya sheria.

# Watoa huduma maji waonywa malimbikizo bili

**Na Timothy Itembe,** TARIME

KATIBU Tawala Wilaya Tarime, Sauli Mwaisenye, amekemea baadhi ya viongozi na watoa huduma za maji wenye tabia ya kuwaongezea wateja wao bili ya maji akitaja vitendo hivyo kuwa kinyume cha sheria.

Alitoa katazo hilo juzi kwenye kikao cha wadau wa maji kilichoandaliwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) cha kukamilisha mwaka kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa miradi ya maji wilayani Tarime.

"Haiwezekani mtu akadaiwa bili ya maji ambayo hajayatumia serikali inakemea vitendo hivyo na kama vipo wilayani hapa vinatakiwa kuachwa mara moja," alisema Mwaisenye.

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Tarime, Mhandisi Mohamed Mtopa, aliishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji husussani mradi kutoka Ziwa Victoria ambao utakuwa suluhisho kwa watumiaji maji.

Alisema hatua za utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Tarime kupitia RUWASA zinaridhisha huku wakiendelea na mazungumza na kampuni ya usambazaji wa mita za kisasa za maji kwa ajili ya kuanza kazi ya kusambaza mita hizo kwa wateja wao.

Ofisa ufuatiliaji tathmini na mafunzo, Enock Edward kutoka WWF alisema kunahitajika elimu kwa watumiaji maji katika suala la kulinda na kutunza miradi na vyanzo vya maji.

Alisema kupitia WWF wanatoa elimu kwa jamii jinsi ya kulinda na kutunza mazingira katika vyanzo vya maji kupitia sheria ya mita 60 kuwa badala ya kukata miti wafuge nyuki na kutaja elimu hiyo kusaidia udhibiti wa uharibifu wa vyanzo vya maji.

Diwani wa Kata ya Sirari, Amosi Sagara alisema, jamii ijengewe uwezo wa elimu ya matumizi ndani ya mita 60 na mamlaka zinazohusika ziweke bikoni na usimamizi makini.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 8 WENYE UHITAJI MKUBWA KUHAMA JANUARI 12 - 13



VICTOR OSIMHEN

# NYOTA WANAOTARAJIWA KUNG'ARA AFCON 2024

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MICHUANO ya 34 ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) itaanza Januari 13, nchini Ivory Coast na kumalizika Februari 11, mwaka huu, jijini Abidjan.

Timu kadhaa za Ligi Kuu ya England zitawakosa nyota wake. Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, atakuwa na nia ya kuchukua kombe la Afrika baada ya kupita miaka 14.

Makala haya inawatazama wachezaji sita ambao wote wanatarajiwa kung'ara kwenye michuano hiyo.

**#1. Mohamed Salah (Misri)**

Mwaka 2022, Misri ilipata kipigo mara mbili kutoka kwa Senegal. Kupoteza fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika kisha kukosa nafasi ya kwenda kucheza Kombe la Dunia huko Qatar.

Mechi zote mbili ziliisha kwa mikwaju ya penalti - na Salah hakupata hata nafasi ya kupiga penalti kwenye fainali ya Afcon, kwani ilibidi asipige tena penalti ya tano.

Taji la mwisho la Misri kati ya mataji yake saba lilikuwa mwaka 2010 na Salah anatazamiwa kufanya vema zaidi kuliko Gabon mwaka 2017 na Cameroon mwaka jana.

Salah ameshinda medali nyingi akiwa na Liverpool, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, atakuwa na nia ya kuongeza mabao katika mechi za Kombe la Mataifa ya Afrika ili kujaribu kuwaongoza 'Mafarao' hao kutwaa kombe hilo.

Akiwa bado na ushawishi mkubwa Anfield msimu huu, "Mfalme wa Misri" atakuwa nahodha wa timu yake dhidi ya Ghana, Cape Verde na Msumbiji katika Kundi B.

**#2. Victor Osimhen (Nigeria)**

Baada ya kutokuwapo katika kikosi cha 2021 kutokana na kuugua Uviko-19 na majeraha. Je, Mchezaji Bora wa Mwaka wa Afrika ataweza kuisaidia Nigeria kushinda taji lao la kwanza tangu 2013?

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amejidhihirisha kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi barani Ulaya, akimaliza msimu uliopita kama mfungaji bora wa Serie A na kuisaidia Napoli kutwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Italia tangu 1990.

Nigeria, bila Osimhen, iliweza tu kutoka sare katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Lesotho na Zimbabwe Novemba. Lakini sasa ana fursa ya kuichezea nchi yake kwenye Afcon.

Mchezaji huyo wa zamani wa Lille alikuwa sehemu ya kikosi cha Super Eagles kwenye fainali za 2019, lakini akatolewa baada ya mapumziko - Nigeria iliposhinda mchujo wa kuwania nafasi ya tatu.

Wababe hao wa Afrika Magharibi wanachuana na Ivory Coast, Equatorial Guinea na Guinea-Bissau katika Kundi A. Kuna tetesi mchezaji huyo atahamia Ligi Kuu England. Je, huu ndio wakati wa Osimhen kujitangaza kwenye anga za kimataifa?

**#3. Serhou Guirassy (Guinea)**

Mshambuliaji huyu amekuwa na mwanzo mzuri msimu huu akiwa na klabu yake ya Stuttgart, amefunga mabao 15 katika mechi 10 za kwanza kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, atashiriki Afcon kwa mara ya kwanza baada ya kucheza mechi yake ya kwanza kwa Guinea Machi 2022.

Katika Kundi C, Senegal, bingwa mtetezi na Cameroon, watampa Guirassy wakati mgumu. Nayo Gambia, iliyofuzu kwa mara ya pili, nayo itaonesha ubabe wake.

**#4. Mohammed Kudus (Ghana)**

Mohammed Kudus alifunga mabao mawili kwa Ghana ilipoilaza Korea Kusini kwenye Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar.

Ghana itasafiri hadi Ivory Coast na itapambana ili isiondolewe katika hatua ya makundi kama ilivyotokea katika Kombe la Mataifa ya Afrika 2021. Ilimaliza kwa kufungwa (3-2) na Comoro.

'Black Stars' hao wamekosa ushindi katika mechi zao mbili za kwanza za kufuzu Kombe la Dunia la 2026. Katika moja ya mechi hizo ilipoteza tena dhidi ya Comoro.

Kudus alikuwa mfungaji bora wa Ghana wakati wa mechi za kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika, akiwa na mabao matatu. Na uwezo wake katika klabu ya West Ham United umeendelea kukua tangu ajiunge na klabu hiyo ya Ligi Kuu England Agosti.

Alifunga mabao mawili kwenye Kombe la Dunia la 2022. Je, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kuisaidia Ghana kurejea kileleni mwa soka la Afrika, ikikabiliwa na mechi ya kwanza ngumu dhidi ya Misri?

**#5. Issa Kabore (Burkina Faso)**

Beki huyo wa kulia anayeshambulia, alichaguliwa kuwa mchezaji bora chipukizi mwaka 2021 na alivutia macho ya wengi pale Burkina Faso ilipoingia nusu fainali, kabla ya kushindwa na mabingwa Senegal.

Kabore alijiunga na Manchester City akitokea Klabu ya Ubelgiji ya Mechelen mwaka 2020, lakini bado anasubiri mechi yake ya kwanza akiwa na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kuwa kwa mkopo nchini Ufaransa katika Klabu za Troyes na Marseille, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, sasa anapata ladha ya kucheza Ligi Kuu England akiwa na Luton Town kwa mkopo, ambayo inapambana isishuke daraja.

Burkina Faso itakapokabiliana na Algeria, Mauritania na Angola katika Kundi D, Kabore, ambaye tayari amecheza mechi nyingi za kimataifa, ana nafasi ya kuonesha uwezo wake ili kujinyakulia nafasi katika timu ya Man City ya Kocha Pep Guardiola msimu ujao.

**#6. Azzedine Ounahi (Morocco)**

Uchezaji mzuri wa kiungo huyo wakati Morocco ikicheza Kombe la Dunia la 2022 - ulichangia kwa kiasi kikubwa uhamisho wake kwenda Olympique Marseille baada ya mashindano hayo.

Hata hivyo, alipata majeraha Machi akiwa na Morocco. Ounahi hakushiriki katika mechi za kufuzu Kombe la Dunia Novemba.

Kocha Walid Regragui amemjumusha kwenye kikosi baada ya kufanya kazi kubwa hadi nusu fainali ya Kombe la Dunia - wakati Morocco itakapomenyana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia na Tanzania katika Kundi F.

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Cristiano Ronaldo juzi wakati Al-Nassr ikishinda 4-1dhidi ya Al-Taawoun kwenye Ligi Kuu Saudi Arabia ni la 54, hivyo linamfanya kuwa mfungaji bora wa mashindano yote kwa klabu na timu ya taifa kwa mwaka 2023, akiwapiku Kylian Mbappe wa PSG na Harry Kane wa Bayern (wenye 52) pamoja na nyota wa Man City, Erling Haaland (50).



# WACHEZAJI 8 WENYE UHITAJI MKUBWA KUHAMA JANUARI



KALVIN PHILLIPS

**LONDON, England**

HAIPENDEZI kuona maisha ya wachezaji yakikwama katika klabu ambayo inaonekana haina mustakabali mzuri kwao, hasa pale wanapojiamini kuwa wana kipaji cha kung'ara kwingine.

Dirisha la uhamisho linawakilisha nafasi kwa wachezaji hawa kukumbusha kila mtu kile wanachoweza na kwa kiwango binafsi zaidi ili waweze kurejea kwenye ubora wao.

Hatuwezi kamwe kujua hasa jinsi mchezaji anajihisi kuhusu kazi yake katika timu ambayo haimpi nafasi, lakini ni wazi haiwezi kuwa na afya bora kwa mtazamo wa akili yake.

Januari hii ni wakati wa dirisha dogo la usajili kwa Klabu za Ulaya na hivyo ni wakati pekee kwa wachezaji kutafuta sehemu wanayoweza kurudisha kiwango chao ili wasogee kwenye kilele cha uwezo wao wa juu.

Makala haya inawaangalia wachezaji nane ambao wanauhitaji mkubwa wa kuondoka wakati huu wa dirisha la hili la Januari.

**#1. Jadon Sancho - Sehemu anayoweza kutua: Borussia Dortmund**

Kama kuna mchezaji aliyehitaji sana mabadiliko ya mazingira basi ni winga wa Manchester United, Jadon Sancho, ambaye maisha yake katika klabu hiyo yanaonekana kukamilika huku Kocha Erik ten Hag akiwa hana mpango naye.

Kurejea kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kunaonekana kuwa chaguo linalowezekana zaidi kwa Sancho - hapo awali aliichezea Borussia Dortmund na yuko kwenye orodha yao ya ununuzi kwa kurejea katikati ya msimu huu. Bayer Leverkusen wanaoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo pia wameonesha nia, kama vile VfB Stuttgart na RB Leipzig, lakini mshahara mnono wa Mwingereza huyo unaweza kumaanisha kurejea BVB ndiyo hatua pekee inayowezekana.

**#2. Kalvin Phillips - Sehemu anayoweza kutua: Newcastle, Juventus**

Kalvin Phillips yuko katika hali sawa na Sancho, tofauti ikiwa ni ukosefu wa taratibu za kinidhamu. Kocha Pep Guardiola amezungumza kuhusu jinsi Phillips anavyofanya mazoezi vizuri na jinsi alivyo mzuri, lakini hilo halijampa nafasi yoyote pale Manchester City.

Ili mchezaji huyo wa zamani wa Leeds United apate nafasi ya kwenda Euro 2024 na England, lazima acheze tu. Juventus wamefanya mazungumzo na City kuhusu uwezekano wa kumnunua kwa mkopo, lakini Newcastle United pia wanamtaka - hatua ambayo inaweza kumfaa zaidi Phillips.

**#3. Noni Madueke - Sehemu anayoweza kutua: Uhamisho wa mkopo EPL**

Noni Madueke aliwasili Ligi Kuu England kutoka PSV Eindhoven Januari 2023 kwa dau la pauni milioni 30, akifuata nyayo za Sancho baada ya kurejea Ligi Kuu baada ya kucheza nje ya nchi.

Kwa bahati mbaya, mchanganyiko wa majeraha, kukosa nafasi na mtafaruku wa jumla ndani ya Chelsea umemfanya Madueke kushindwa kufanya vizuri. Alifunga penalti ya ushindi katika ushindi mdogo dhidi ya Crystal Palace katikati ya wiki iliyopita, lakini nafasi zimekuwa chache chini ya kocha Mauricio Pochettino.

Ingawa Chelsea inaonekana bado kumhitaji, lakini Madueke anahitaji kitu kutokea haraka katika Maisha yake.

**#4. Aaron Ramsdale - Sehemu anayoweza kutua: Chelsea, Newcastle United**

Kabla ya wiki za mwisho za dirisha la usajili la majira ya joto, isingekuwa jambo la kufikiria kuwa Aaron Ramsdale anaweza kuwa anataka kuondoka Arsenal.

Alicheza nafasi kubwa katika kusukuma mbele nia ya kusaka taji la Ligi Kuu kwa 'Washikabunduki' hao msimu uliopita - licha ya kufanya makosa machache njiani.

Lakini ujio wa David Raya kutoka Brentford ulimfanya kuwa na nafasi finyu, ingawa Mikel Arteta alidai kwa ujasiri kuwasili kwake hakuashirii mabadiliko. Hakika, Ramsdale nafasi yake imebadilishwa.

Chelsea na Newcastle zote zimeonesha nia ya kumtaka Mwingereza huyo, lakini Arsenal hawana uwezekano wa kumruhusu kuondoka hadi majira ya joto.

**#5. Eric Dier - Sehemu anayoweza kutua: Sporting CP, Ligi Kuu Saudia**

Ina maana kwamba Eric Dier huenda hatahama Januari, lakini kuna uwezekano wa kutamani mabadiliko ya mandhari baada ya kuanguka chini pale Tottenham Hotspur.

Micky van de Ven amejitambulisha kama mshirika mzuri zaidi wa Romero chini ya Kocha Ange Postecoglou, huku Muaustralia huyo akiwapa nafasi ya beki wa pembeni Ben Davies na Emerson Royal katika majukumu ya muda.

Hilo linahitimisha sana hali ya Dier, Ligi Kuu ya Saudi Arabia inaonekana kuwa salama kwake baadaye mwakani.

**#6. Divock Origi - Sehemu anayoweza kutua: AC Milan, Ligue 1**

Kazi ya Divck Origi imekuwa ya kuvutia. Alifanikisha ndoto ya kila mwanasoka, kufunga bao kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa Liverpool wakati wakibeba taji hilo, lakini ametumia muda mwingi sana kwenye benchi kwa mchezaji ambaye amethibitishwa kuwa na ujuzi wa kufunga mabao.

Watu wengi watakuwa wamesahau kwamba Origi yuko Nottingham Forest, baada ya kuhama kwa mkopo msimu wa majira ya joto, na kuna uwezekano mkubwa kwamba dili hilo litakatizwa Januari ili kumrudisha Milan.

**#7. Ferran Torres - Sehemu inayowezekana kutua: Arsenal**

Ukitazama kwa haraka dakika za Ferran Torres pale Barcelona na unaweza kufikiria ni kweli anahitaji kuondoka Katalunya? Jibu ni ndio, Mhispania huyo anahitaji hivyo.

Barca wamebarikiwa kuwa na chaguo pana na amekuwa akicheza kikosi cha kwanza mara kwa mara, ni wazi kwamba hana nafasi katika timu hiyo. Kuibuka kwa Lamine Yamal kumefanya mambo kuwa magumu zaidi na Torres anaonekana kuwa zaidi ya kigingi cha mraba katika chaguo la shimo la duara, akizuiliwa wakati mambo mengine hayafanyiki.

Tena, kuondoka Januari kunaweza kusitimie - ana uzoefu wa kufanya hivyo siku za nyuma - na inabaki kuona kama Arsenal inayomtaka kwa muda mrefu itaweza kumsajili.

**#8. Malang Sarr - Sehemu anayoweza kutua: OGC Nice**

Aliyejificha kwenye korido za Stamford Bridge ni Malang Sarr - mchezaji aliyeiwakilisha Ufaransa katika kila ngazi ya vijana.

Kuwasili mwaka 2020 kutoka OGC Nice, beki huyo wa kati kwa sasa mwenye umri wa miaka 24, hajawahi kupewa nafasi Chelsea na itawashangaza wengine kujua kwamba bado yumo kwenye vitabu vya kukusanya mshahara wake.

Porto na Monaco walimtumia Sarr kwa mkopo siku za nyuma, lakini hakuweza kuwashawishi kufanya mambo kuwa ya kudumu. Klabu ya zamani ya Nice inaweza kuwa na nia.

## Nukuu

"Hakuna timu inayoweza kukabiliana na majeruhi wengi," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, baada ya juzi kukubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Nottingham Forest**



"Hatuko juu, lakini sikutarajia hilo kutokana na matokeo tuliyopata. Mbali na michezo miwili au mitatu, tulicheza vizuri sana bila matokeo ambayo labda tulistahili - lakini kwenye soka kile unachostahili hakihesabiki, ni biashara na lazima ushinde michezo - na hapa tulifanya hivyo," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baada ya ushindi wa mabao 2-0 juzi dhidi ya Sheffield United.**



"Tutachukulia kila mchezo kama fainali," **Kocha wa Timu ya Taifa ya Misri, Mreno Rui Vitoria kuelekea fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON**.






KIBU DENIS

# WACHEZAJI WA5 LIGI KUU WALIORUDI KWENYE UBORA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA utakuwa mfuatiliaji wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara misimu ya nyuma pamoja na viwango vya wachezaji, utagundua baadhi yao msimu huu wamerejea kwenye viwango vyao vilivyozoeleka.

Tena wengine wako kwenye viwango vya juu zaidi kuliko hata walivyokuwa navyo mwanzo. Baadhi ya wachezaji walionekana kushuka viwango kiasi cha kuanza kubezwa na mashabiki wa soka, huku wachambuzi wakitabiri kuwa wanaweza kuoneshewa mlango wa kutokea.

Hata hivyo, mpaka kufikia raundi ya 14 ya Ligi Kuu, baadhi ya wachezaji wameonekana kurejea kwenye viwango vyao ambavyo vilishuka kwa sababu mbalimbali, lakini kwa sasa hawashikiki, wapo juu kama moto wa kifuu.

Katika makala haya, tunakuletea wachezaji watano ambao walionekana kushuka na kupoteza namba zao lakini sasa warejesha kila kitu...

**1. Stephane Aziz Ki - Yanga**

Ndiye mchezaji aliyesajiliwa na kutambulishwa kwa mbwembwe nyingi msimu uliopita. Alitambulishwa usiku wa manane na klabu yake ya Yanga, ikidaiwa kuwa ulikuwa ni usajili wa pesa nyingi uliovunja rekodi.

Muivorian huyo, alianza ligi kwa moto mkali, lakini pamoja na debe kubwa alilopigiwa, baadaye alianza kuonekana mchezaji wa kawaida kiasi cha kila mmoja kuanza kubeza na kudhani huenda msimu huu asingekuwapo kwenye timu yake.

Kocha aliyepita, Nasreddine Nabi alianza kumweka nje kwenye baadhi ya mechi na akawa anaingia akitokea benchini.

Si kwamba alikuwa mbaya sana, lakini hakuwa na mwendelezo sahihi wa kiwango chake kwani alikuwa 'maji kupwa, maji kujaa.'

Pamoja na kwamba alifunga mabao tisa kwenye Ligi Kuu, lakini kwa jinsi alivyokuwa anaimbwa, bado hata baadhi ya Wanayanga hawakuridhika.

Msimu huu amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na sasa ndiye watu wanatambua kwa nini alitambulishwa usiku wa manane.

Ndiye mhimili mkubwa kwa Yanga kwa sasa, akiwa ameshapachika mabao 10 na 'assist' mbili, wakati ligi ikiwa kwenye raundi ya 14, ikibaki mechi moja imalize mzunguko wa kwanza, lakini timu yake ikiwa ndiyo kwanza imecheza mechi 11 tu. Kwa sasa anaongoza katika orodha ya wapachika mabao Ligi Kuu, manane akifunga kwa mguu wa kushoto na mawili mguu wa kulia.

**2. Kibu Denis - Simba**

Ni msimu uliopita tu ambapo hakuna mwanachama na shabiki wa Simba aliyekuwa akitaka Kibu Denis abakie klabuni hapo. Baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu msimu wa 2021/22, kila mmoja alidhani angepelekwa kwa mkopo sehemu yoyote ile.

Kwa kudra za Mwenyezi Mungu tu, akabaki kikosini licha ya kelele nyingi za kutaka aachwe. Alikiwasha kisawasawa akiwa kwenye Klabu za Geita Gold na Mbeya City kiasi cha kuitwa Timu ya Taifa, Taifa Stars baada ya kupewa uraia.

Mambo yalibadilika alipojiunga na Klabu ya Simba 2021 ambapo aling'ara kwenye mechi za mwanzo tu, baada ya hapo ikawa hadithi ya kusikitisha.

Kocha Mkuu Roberto Oliveira 'alichekesha walionuna', alipojiunga na kikosi cha Simba nchini Uturuki na kusema mchezaji aliomkosha kiasi cha kumpa zawadi ni Kibu. Si mashabiki wa soka, hata Wanasimba wenyewe walimshangaa kocha wao.

Panapo ukweli uongo hujitenga, hivi tunapozungumza Kibu ndiye mchezaji anayependwa zaidi na mashabiki wa Simba kuliko yeyote yule. Hafungi sana mabao, lakini tangu msimu uliopita hadi huu, ndiye mchezaji anayecheza kwa kujituma zaidi kuliko mwingine kwenye kikosi hicho, alionekana kuwa na utimamu wa mwili wa hali ya juu kuliko wote, na mwenye kuipambania nembo ya klabu kiasi cha sasa kuonekana kuwa mfano kwa wengine.

Anakimbia, anakaba, hampishi mtu, na ndiye mchezaji ambaye akichukua mpira anapasua ngome na kulitafuta lango, badala ya kutoa pasi za pembeni. Amehusika katika mabao mengi ya Simba, ambapo kama siyo 'assist', basi shambulizi litakuwa lilianzia kwake.

**3. Fei Toto - Azam**

Mgogoro wake na klabu yake ya zamani, Yanga ulimfanya asiwe uwanjani kwa muda mrefu.

Kabla ya hapo, Feisal Salum 'Fei Toto', alikuwa ni mmoja wa wachezaji tegemeo ambao walikuwa na uwezo wa kuamua mechi yoyote ngumu, akikupa mabao anayoyafunga kwenye mazingira magumu.

Kwa msaada mkubwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Muungano, Dk. Samia Suluhu Hassan, Fei Toto alirejea uwanjani, lakini safari hii akiwa na jezi ya Azam FC mwanzoni mwa msimu huu.

Awali, alionekana kuzidi mwili, kiasi cha kuonekana kama anacheza kizembezembe hivi, lakini kadri muda ulivyozidi alionekana kurejea kwenye kiwango chake kiasi haikushangaza kuitwa Taifa Stars.

Na si hivyo tu, ameanza kuweka rekodi ambazo hajawahi kuziweka huko nyuma, hivyo kiwango chake cha msimu huu kimezidi hata alivyokuwa huko nyuma kitakwimu.

Ameshapachika mabao manane mpaka sasa kwenye Ligi Kuu kabla ya mzunguko wa kwanza kumalizika, akiwa na 'assist' nne.

Fei Toto anaongoza kwa kusaidia jumla ya mabao 12 kwenye kikosi cha Azam, akiwa sawa na Aziz Ki wa Yanga.

**4. Waziri Junior - KMC**

Ligi Kuu ya msimu wa 2019/20 wakati straika Mnyarwanda Meddie Kagere akitwaa Kiatu cha Dhahabu na mabao yake 22, Waziri Junior alishika nafasi ya pili akimaliza msimu huo na mabao yake 14 akiwa na Klabu ya Mbao FC.

Baada ya msimu kumalizika, Yanga ilimdaka mchezaji huyo ikiwa na matumaini ya kumuona akiendelea kuuwasha moto kama alivyofanya.

Haikuwa hivyo, kiwango chake kiliporomoka ghafla na kufunga bao moja tu msimu wa 2020/21.

Ni mmoja wa wachezaji ambao anaweza kucheza msimu mmoja vizuri, halafu akakuangusha msimu ujao, kwani 2017 alikuwa Toto African akauwasha kweli kweli hadi akasajiliwa na Azam FC msimu wa 2017/18, lakini hakuonesha makali, akatimkia Biashara United ambako nako hakuwa na msimu mzuri 2018/19, kabla kwenda Mbao FC na akawa kwenye kiwango cha juu msimu wa 2019/20 ambapo Yanga ilimuona.

Msimu huu, straika huyo mzawa amekuja kivingine. Ana mabao saba mpaka sasa ambapo ligi ipo kwenye raundi ya 14, akiichezea Klabu ya KMC.

Ndiye aliyefunga mabao yote mawili dhidi ya Simba na kuiongoza timu yake ya KMC kutoka sare ya 2-2.

**5. Prince Dube - Azam**

Kesi yake huyu staa ni majeraha tu. Kuna wakati anakuja juu, lakini akitoneshwa anakaa nje kwa muda na hata anaporejea hawi kwenye kiwango chake cha kawaida hadi baada ya muda fulani. Ndiyo maana kuna wakati amekuwa hayupo kwenye kiwango bora na nyakati nyingine anakuwa tishio kwenye ligi.

Mzimbabwe huyu, hajawahi kuwa tishio sana kwenye kinyang'anyiro cha ufungaji bora kutokana na kutomaliza msimu bila kuumia, lakini kipindi anachokuwa kwenye ubora ni mmoja kati ya mastraika hatari nchini.

Msimu huu ameonekana kuwa kwenye ubora wa hali ya juu kuliko uliopita, akiwa ameshapachika mabao sita.

Kama hatoumia kama inavyokuwa, basi msimu huu ni mshindani mkubwa katika kuwania Kiatu cha Dhahabu.

**JE, WAJUA?**



HADI sasa msimu huu, Manchester United imepoteza michezo mingi (14) kuliko waliyoshinda (12) katika mashindano yote. Lakini ni mwaka 1930 (28), 1972 (25) na 1921 (24) tu ndio walipoteza michezo mingi zaidi katika mwaka wa kalenda kuliko vipigo 21 walivyopata mwaka 2023.





# Huduma za afya zaimarika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bestie Magoma, amesema hali ya upatikanaji huduma bora za afya mkoani hapa imeendelea kuimarika baada ya kuongezeka kwa vituo vya afya.

Akizungumza jijini hapa wakati wa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa, Dk. Magoma, alisema hali hiyo imetokana na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 429 mwaka 2021 hadi kufikia 545 Novemba mwaka huu.

Alisema idadi ya vituo ambavyo vimeanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji wa dharura katika mkoa ni 47 kwa hospitali 14 na vituo vya afya 33.

Katika eneo la huduma za uchunguzi wa magonjwa, Dk. Magoma alisema zimeendelea kuimarika hivyo kupunguza rufani za kiuchunguzi kwa wagonjwa.

"Na hii imetokana na kusimikwa kwa mashine za kisasa za uchunguzi," alisema.

Alisema mkoa umeweza kufikia lengo la asilimia 124 kwa utoaji wa chanjo tatu muhimu kwa watoto chini ya miaka mitano.

Alisema pia mkoa unatekeleza mikakati inayolenga kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara katika vituo vya afya na kuongeza upatikanaji wa dawa kufikia asilimia 91 hadi Novemba mwaka huu.

Kwa mujibu wa Dk. Magoma, kumekuwa na ongezeko la bajeti iliyotolewa na Serikali Kuu ya ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa Kanda ya Dodoma hadi kufikia Shilingi bilioni 18.772 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema katika kipindi cha Julai hadi Novemba mwaka huu, bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 2.549 zimesambazwa katika halmashauri huku mkoa ukipokea shilingi bilioni 5.1 kupitia halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika zahanati, vituo vya afya na baadhi ya hospitali za wilaya kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24.

**Katika eneo la huduma za uchunguzi wa magonjwa, Dk. Magoma alisema zimeendelea kuimarika hivyo kupunguza rufani za kiuchunguzi kwa wagonjwa.**

# Wafanyakazi walala nje ya ofisi ya RC Dodoma

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ZAIDI ya wafanyakazi 50 wa Kampuni ya Ujenzi ya Judex Contractors Ltd wamelala nje ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kumshinikiza mwajiri wao kulipa Shilingi milioni 39 baada ya kuchimba mitaro katika mradi wa maji Wilaya ya Chamwino.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Emmanuel Joseph alisema kuwa kutokana na kutolipwa stahiki zao kwa wakati wanakabiliwa na hali ngumu ya maisha baada ya kufukuzwa kwenye nyumba waliyokuwa wakiishi iliyopo Kijiji cha Haneti unakotekelezwa mradi huo.

Joseph alisema tangu kuanza kwa mradi huo, walilipwa Shilingi milioni 11 na kwa sasa wanadai kiasi hicho cha Shilingi milioni 39 baada ya kazi hiyo kukamilika tangu Desemba Mosi mwaka jana.

Alisema walianza kuchimba mtaro kwenye mradi huo wa maji katika Kijiji cha Haneti Oktoba 23, mwaka jana.

Joseph alisema mapatano yao ilikuwa ni kuchimba mtaro mita moja kwa Shilingi 1,500 na kwamba walichimba kilomita 25 kwa thamani ya Shilingi milioni 50.

Mkurungenzi wa Judex Contractors Ltd, Judith Odunda, akiongea kwa njia ya simu, alithibitisha kudaiwa kiasi hicho cha fedha na wafanyakazi hao.

Judith alisema kutokana na kazi iliyofanyika Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) walitakiwa kumlipa Shilingi milioni 80 hadi atakapotandaza mabomba.

Alisema kwa sasa yupo kwenye mchakato wa kutafuta fedha za kununulia mabomba hayo na kuwalipa wafanyakazi hao.

Alisema aliwalipa Shilingi milioni tano hivi karibuni kama nauli na kuwaomba warudi nyumbani na kuahidi kuwa atawatumia stahiki zao kila moja kwa sababu ana mawasiliano yao ya simu.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari mjini Musoma mwishoni mwa wiki na kuwataka watumishi wa umma kutokuwa kikwazo cha utoaji wa taarifa kwa vyombo vya habari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi watangaziwa kiama

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WAZAZI wilayani hapa wameagizwa kuwapeleka watoto wao wanaostahili kuanza darasa la kwanza na wale waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kwa msimu wa masomo wa mwaka huu wa 2024, lasivyo watakamatwa na kufikishwa mahakamani.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Dk. Omary Nkulo, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake wilayani hapa.

Dk.Nkulo alisema wazazi hao wanatakiwa kuhakikisha wanawaandaa watoto wao wanaotakiwa kuanza masomo kabla ya shule kufunguliwa Januari 8, mwaka huu.

Alisema baada ya shule kufunguliwa watafanya msako kwa kupita nyumba hadi nyumba kwa lengo la kujiridhisha kama watoto wote wamepelekwa shule.

Dk. Nkulo alionya kuwa wazazi watakaokaidi agizo hilo la Serikali la kuwapeleka watoto wao shule watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kukamatwa na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Aliyataja baadhi ya maandalizi wanayostahili watoto hao kuwa ni pamoja na wazazi kuwanunulia viatu, vitabu, madaftari, sare na kwa wanafunzi wa bweni wa sekondari vifaa vyote ambavyo wameelekezwa kwenye fomu.

Alisema uongozi wa halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Waratibu Elimu Kata, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanaendelea kupita nyumba hadi nyumba kuwaandikisha watoto wenye umri wa kuanza darasa la kwanza kwa shule za msingi.

Alisema matarajio yao ni kuandikisha zaidi ya watoto 14,303 kwa darasa la awali na la kwanza 13,931.

Vilevile alitangaza kiama kwa wazazi wenye wanafunzi watoro kuwa nao watachukuliwa hatua za kisheria kwa kuwaacha wanakaa nyumbani bila ya kwenda shule.

"Agizo hili linaenda sambamba na wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kwa kuwa nao wanatakiwa kuandaliwa mapema ili kufika wakati kwenye shule walizopangiwa," alisema na kusisitiza kuwa:

"Siku ya kufungua shule wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti bila kuchelewa na kama kuna tatizo litashughulikiwa baada ya mwanafunzi kuripoti shuleni."

Akizungumzia kuhusu maeneo ya wafugaji, alisema wamefanya mikutano ya kuwaelimisha umuhimu wa elimu na wameanza kuandikisha watoto bila kipingamizi.

Dk. Nkulo alisema serikali ya awamu ya sita imejenga shule kila mahali, hivyo hakuna kisingizio cha umbali wa shule kutoka kwenye maeneo wanakoishi wanafunzi hadi shuleni.



# Magereza yaagizwa kukarabati Chuo Kiwira

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

SERIKALI imeliagiza Jeshi la Magereza nchini kutenga fedha katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Magereza Kiwira, wilayani Rungwe ili kiendane na hadhi ya chuo.

Aidha, jeshi hilo limeagizwa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Shule ya Msingi Chuo cha Magereza Kiwira iliyopo ndani ya eneo la chuo ambayo asilimia kubwa ya wanafunzi ni watoto wa maaskari.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alipokuwa anafunga mafunzo ya awali ya askari 734 wa jeshi hilo kuwa chuo hicho ni muhimu kwa taifa.

Alisema baada ya fedha kupatikana ukarabati unatakiwa kuanza mapema na atahakikisha anafuatilia utekelezaji wa maagizo hayo ili chuo hicho ambacho ni pekee cha mafunzo ya awali nchini kiwe na hadhi inayoridhisha.

"Kama Mungu atajaalia niendelee kuwa katika wizara hii, nitakuja mwishoni mwa mwaka 2024 kuja kukagua utekelezaji wa maagizo haya, chuo hiki ni muhimu sana kwa taifa letu, lakini pia ile shule ndiyo inayotufundishia watoto wetu hapa," alisema Waziri Sagini.

Kuhusu askari waliohitimu mafunzo, aliwataka kwenda kufanya kazi kwa weledi kwenye maeneo watakayopangiwa ili walisaidie taifa kupata maendeleo. Aliwataka kuzingatia miiko ya kazi yao watakapokuwa wanatekeleza majukumu ili kuepuka kufanya makosa yatakayowasababishia matatizo na watu wengine.

Akitoa taarifa ya chuo hicho, Kamishna Jenerali wa Magereza nchini (CGP), Mzee Ramadhan Nyamka, alisema wanakusudia kuvifanyia ukarabati vyuo vyote vya Magereza nchini ili viwe katika hali nzuri na inaoendana na umuhimu wa jeshi hilo.

Alisema miundombinu ya vyuo vyote vya jeshi hilo viko katika hali isiyoridhisha na kutegemea kuanza ukarabati katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Alisema miundombinu ya vyuo inakabiliwa na matatizo mengine madogo ambayo wanayatatua kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Tunataka kuvikarabati vyuo vyetu vyote ili askari wetu wapate mafunzo katika mazingira ambayo yanaridhisha, tutafanya ukarabati huu kulingana na upatikanaji wa fedha utakavyokuwa," alisema CGP Nyamka.

Mkuu wa Chuo cha Magereza Kiwira, Kamishna Msaidizi wa Magereza (ACP), Fredrick Wambura, alisema askari waliohitimu mafunzo hayo ya awali wamepatiwa maarifa mbalimbali yanayohusu kazi yao.

Alisema kati ya askari hao 734 waliohitimu mafunzo, 526 ni wa wanaume na wa kike ni 228 na wahitimu wote wamepata maarifa yanayofanana.

Wahitimu hao walijifunza sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu kazi hiyo na walionyesha umahiri wa kujifunza kwa nadharia na vitendo.

Baadhi ya wahitimu waliahidi kwenda kufanya kazi kwa weledi hasa katika kutekeleza jukumu lao la kurekebisha tabia za watu wanaokuwa wametenda makosa.

Mmoja wa wahitimu hao, Janeth Sinda alisema kwenye mafunzo hayo walifundishwa misingi mbalimbali ya kazi hiyo na kwamba watahakikisha wanatimiza majukumu kwa kuzingatia misingi hiyo pamoja na kusimamia viapo.




Mafundi wanaojenga barabara ya njia nne yenye urefu wa kilomita 29 kutoka Nsalaga jijini Mbeya kwenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, wakiendelea na ujenzi wa mtaro katika eneo la Mwakapangala, Mji wa Mbalizi mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# WanaKyela watoa msaada kwa wenye ualbino

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

UMOJA wa wazawa wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, waishio ndani na nje ya wilaya hiyo (Kyela Ibasa Festival), wametoa msaada wa mafuta ya kupaka na miwani kwa watu wenye ualbino.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi na Mwenyekiti wa Kamati ya Jamii, Vanessa Nyesyenge kwa niaba ya Wanaibasa ambao kwa umoja wao walichangishana fedha kwa ajili ya kuisaidia jamii ya wilaya yao ikiwa ni utaratibu waliojiwekea kila inapofika mwisho wa mwaka kusaidia sekta ya afya, elimu, kuenzi utamaduni kwa kuandaa ngoma za asili na kutembelea vivutio vya utalii ikiwamo fukwe ya Matema Beach.

Watu 35 wenye ualbino walipatiwa mafuta maalum kwa ajili ya kuwasaidia kuwakinga na ngozi pamoja na miwani kwa wale wenye matatizo ya macho ambao wanapimwa na kupatiwa.

Akipokea msaada huo, Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ualbino Wilaya ya Kyela, Bwigane Mwamasangula, alisema walikuwa wanakabiliwa na tatizo kubwa la ngozi kwa sababu ya kukosa mafuta hasa kipindi hiki cha jua kwa sababu ya kukosa fedha ya kununua bidhaa hiyo.

Alisema yatawasaidia kulinda na kutunza ngozi zao pamoja na miwani waliyopewa, lakini aliuomba umoja huo kuendelea kuwasaidia kwa sababu hawana fedha za kudumu gharama za mafuta hayo ambayo walitoa ambayo alidai yanauzwa kwa bei ghali.

"Tunawashukuru sana Ibasa kwa msaada huu hakika mnarudisha fadhila nyumbani, kutokana na hali zetu duni tumeshindwa kabisa kumudu gharama za ununuzi wa mafuta ya kulinda ngozi zetu wilaya yetu ni ya joto na jua kali kwa hali zetu tunajikuta tunapata mateso sambamba na miwani asilimia kubwa sisi macho yetu yanashida hivyo miwani mliotupatia itatusaidia sana, tunaomba mwendelee kutukumbuka," alisema Mwamasangula.

Katika hatua nyingine Kyela Ibasa imetoa msaada wa vifaa tiba, vitendanishi na mashuka 20 kwa ajili ya Zahanati ya Njisi kwa ajili ya kusaidia upatikanaji bora wa huduma za matatibu.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Njisi, Johson Mganyizi, alisema msaada huo utasaidia kuondoa tatizo ya uhaba wa vifaa tiba ambavyo licha ya serikali kuvinunua lakini mahitaji yamekuwa makubwa kutokana na kituo hicho kuhudumia idadi kubwa ya wananchi.

Sh. milioni 4.9 zilitolewa na Kyela Ibasa kwa ajili ya kusaidia jamii katika sekta ya afya ambapo walitoa mashuka, vifaa tiba, vitendanishi, mafuta na miwani kwa ajili ya watu wenye ualbino pamoja na sekta ya elimu kwa kununua vitabu ya masomo mbalimbali kusaidia watoto wanaosoma Shule ya Sekondari Njisi.

## Anaswa akitaka kusafirisha bangi kutoka Malawi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Kelvin Amanyisye, mkazi wa Lubele, Wilaya ya Kyela mkoani humo kwa tuhuma za kukutwa na bangi akitaka kusafirisha kwenda jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali zinazofanywa na jeshi hilo kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema kijana huyo alikamatwa akivusha bangi hiyo yenye uzito wa gramu 13 kutoka nchi jirani ya Malawi kupitia kipenyo kisicho rasmi kiitwacho Boda ya zamani.

Alisema kijana huyo alikuwa amehifadhi bangi hiyo kwenye mifuko ya plastiki aina ya Rambo kisha kuiweka kwenye begi kubwa kwa nia ya kusafirisha kwa njia ya basi.

"Alikuwa amepakia kwenye pikipiki na alikuwa anapeleka kwenye stendi ya mabasi ya Kyela ili apakie kwenye basi kuelekea jijini Dar es Salaam," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema wanaendelea kumhoji kijana huyo kwa ajili ya kupata taarifa zaidi kuhusu biashara hiyo ikiwamo kuwabaini watu wengine wanaoshirikiana naye.

Alisema baada ya kukamilisha upelelezi wataendelea na hatua zingine ikiwamo kumfikisha mtuhumiwa mahakamani huku akiwataka vijana kufanya kazi halali na kuachana na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Aliitaka jamii kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kutokomeza biashara ya dawa hizo kwa kutoa taarifa za siri kuhusu watu wanaoziuza akisisitiza kuwa zina madhara makubwa.



## SMZ inavyoandaa vijana kupata ajira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inafanya juhudi kuwaandaa vijana kielimu kwa lengo la kuimarisha uchumi nchini na kukabiliana na ushindani katika soko la ajira duniani.

Othman aliyasema hayo juzi wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la shule ya sekondari ya ghorofa katika Kijiji cha Kojani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba utakaogharimu zaidi ya Shilingi bilioni 3.3 pamoja na samani.

Alisema SMZ imeweka kipaumbele suala la elimu kwa maendeleo ya nchi kwa kuwa bila elimu hakuna maendeleo katika taifa lolote duniani.

Alisema pia inatekeleza mpango mkubwa wa mageuzi ya elimu ili kuwe na nafasi ya kutosha kwa vijana kusoma katika mazingira ya kuvutia.

Alisema kupitia mpango wa mageuzi ya elimu, SMZ inakusudia kuanza majaribio ya utekelezaji wa mtaala mpya wa sekondari ili kuimarisha ujuzi wa vijana kulingana na soko la ajira duniani.

Alisema ni vema serikali na wazazi kushirikiana kuwaandaa vijana kwa elimu kulingana na maarifa ya ajira katika soko lolote duniani kwa kuwa ina msukumo mkubwa wa nchi nyingi ambazo zina mazingira kama ya Zanzibar.

Alisema kuna dhana kuwa vijana wameandaliwa kufanya kazi katika taasisi kupitia ushindani wa kidunia.

Hata hivyo, Othman alisema ufanisi wa jitihada hizo katika utoaji wa elimu bora nchini, kutategemea ushirikiano kutoka kwa wazazi wa kubeba jukumu lao la kufuatilia vijana wao.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema wanafarijika na jitihada za serikali kuongeza majengo ya ghorofa katika kuimarisha sekta ya elimu nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, alisema ujenzi wa majengo mapya ya shule ni jitihada za serikali za kuboresha elimu kupitia miundombinu ya madarasa na maabara za kisasa.

# Ufaulu mitihani darasa la nne, saba wapanda Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani Zanzibar limetangaza matokeo ya mitihani ya taifa ya darasa la nne na saba kwa mwaka huu yakionyesha ufaulu umepanda kwa asilimia 1.69 ikilinganishwa na wa asilimia 89.66 wa mwaka jana.

Akitangaza matokeo hayo jana kwa waandishi wa habari katika ofisi za Wizara ya Elimu zilizopo Mazizini visiwani hapa, Mkurugenzi wa baraza hilo, Othman Omar Othman, alisema katika matokeo hayo watahiniwa 233 wenye mahitaji maalum wamefaulu, wakiwamo wasioona wawili, uoni hafifu 56, wa kusikia 19, viungo 12, akili 14 na mchanganyiko 30.

"Watahiniwa wote wenye ulemavu waliosajiliwa kufanya mitihani ni 238 kati yao wasiona wanne, uoni hafifu 93, viziwi 36, wenye ulemavu wa akili 68, walemavu wa viungo 16 na ulemavu mchanganyiko 21," alisema.

Kwa mujibu wa Othman, Somo la Sayansi na Teknolojia lina asilimia kubwa 95.40 ya waliofaulu, likifuatiwa na Dini na Kiarabu 91.68, Kiswahili 76.28, Kiingereza 75.41 na Hisabati 73.70.

Alisema jumla ya watahiniwa 44,726 wa darasa la saba walisajiliwa kufanya mitihani hiyo, kati yao, wavulana ni 21,465 sawa na asilimia 47.99 na wasichana 23,261 sawa na asilimia 52.01, waliofanya mitihani hiyo ni asilimia 97.42.

Alisema watahiniwa 41,396 sawa na asilimia 95.00 kati ya 43,574 walifanya mitihani hiyo, wamefaulu kwa daraja la A,B,C,D na watahiniwa 2,178 sawa na asilimia 5.00 wamepata daraja F.

"Ufaulu huu umepanda kwa asilimia 8.58 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 86.42 kwa mwaka 2022," alisema mkurugenzi huyo.

Hata hivyo, alisema watahiniwa 308 wamefaulu vipaji maalum kwa kupata alama daraja A, watahiniwa 6,358 wa michepuo wamepata daraja B na 17,183 daraja C.

Alisema katika mwaka huu wa 2023 Somo la Ubunifu na Sanaa na Michezo lina ufaulu mzuri kwa kuwa na asilimia kubwa 99.86 ya watahiniwa waliofaulu huku la hisabati likipata ufaulu mdogo wa asilimia 50.10.

"Katika mtihani huu, wanatahiniwa 2,356 sawa na asilimia 4.02 hawakufanya mitihani kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ugonjwa kati yao, wavulana 1,618 na wasichana 738.




Baadhi ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi wakishiriki ujenzi wa nyumba ya kitega uchumi cha UVCCM Mkoa wa Kaskazini Pemba. **PICHA: IS-HAKA OMAR**

# Maofisa vikosi vya ulinzi kuboreshewa mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar (SMZ) imetangaza mpango wake wa kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa maofisa na wapiganaji wa vikosi vya ulinzi na usalama visiwani hapa ili kufikia malengo ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Mpango huo ulitangazwa jana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, wakati akifungua jengo la ofisi ya utawala ya Kikosi cha Kuzuia Majengo Zanzibar (KMKM) Kamandi ya Kusini Unguja lililopo eneo la Ungu Ukuu Wilaya ya Kati.

Akizungumza katika hafla hiyo ambayo ni mwendelezo wa shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Abdulla, alisema SMZ itaendelea kuimarisha miundombinu kwa vikosi vya ulinzi na usalama KMKM ili kuendana na mabadiliko yanayoendelea kutokea duniani na kuwajengea uwezo na utayari wa ulinzi raia na mali zao.

Alisema dhana ya Mapinduzi ni kuwaletea maendeleo wananchi visiwani hapa bila ya ubaguzi, kuimarisha ulinzi wa nchi, rai ana mali zao na taasisi za serikali na wafanyakazi wafanye kazi kwa ufanisi.

Alikitaka KMKM kutunza jengo hilo na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na serikali, viongozi kuwajibika, kutenda haki kwa kulinda raia na mali zao na kuhakikisha wanapambana wanaohujumu uchumi kwa kusafirisha bidhaa kwa njia ya magendo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Vikosi Maalum vya SMZ, Issa Mahfoudh Haji, alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Shilingi bilioni 1.1 ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili maofisa na askari wa kikosi hicho.

Haji, alisema mradi huo ni mwendelezo wa ujenzi wa majengo ya ofisi, nyumba na mahanga ya wapiganaji visiwani hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, aliwataka askari na maofisa hao wa KMKM kuhakikisha wanapambana na watu wanaojihusisha na usafirishaji magendo na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

# Rais Samia awakumbuka wazee kambi ya Misufini

**Na Steven William, MUHEZA**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa msaada wa vyakula kwa wazee wanaoishi katika kambi ya Misufini, Kijiji cha Umba wilayani Muheza, mkoani Tanga kwa ajili ya kuwatakia heri ya Sikukuu ya Mwaka Mpya.

Akikabidhi msaada huo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, aliwataka wazee katika kambi hiyo kuishi kwa amani na upendo.

Alisema Rais Samia anawathamini wazee na anapenda waishi maisha mazuri kama watu wengine wa kitanzania, huku akiitaka jamii kushiriki kuwahudumia wazee hao ili waweze kutimiza ndoto zao.

"Rais Samia anawajali Watanzania wote na amewiwa kutoa sadaka hii unga wa sembe na mafuta ya kupikia na mbuzi kwa ajili yenu, anataka mjisikie wenye furaha katika kusherehekea Sikukuu ya Mwaka Mpya kama watu wengine," alisema Mfaki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, alisema Rais Samia amegus wa na uhitaji wa wazee na ndiyo maana ametoa msaada huo.

Naye Mwenyekiti wa Wazee, Joseph Misigalo, alimshukuru Rais kwa msaada huo na kumwomba aendelee na moyo huo wa upendo wa kuwajali wazee.

Msaidizi wa Afya Mkuu katika kambi hiyo, Hashim Mwanyoka, alisema wamefurahishwa na kitendo hicho cha kiungwana kilichofanywa na Rais Samia, kwamba msaada huo utawasaidia wazee hao katika sherehe ya Sikukuu ya Mwaka Mpya.

Ofisa Mfawidhi na msimamizi wa makazi katika kambi hiyo, Mwamvita Kilima, alisema wanafarijika sana pale wanapoona serikali na hasa kiongozi mkubwa kama Rais anawakumbuka wazee wanapata amani.

Alisema kuwa katika kambi hiyo wanakabiliwa na tatizo la ubovu wa barabara kutoka katika Kijiji cha Umba mpaka kufika kambini hapo, kwamba maji yanapita juu ya daraja ambalo limebomoka watoto wanashindwa kwenda shule kipindi cha mvua.

Alisema kuwa kuna tatizo lingine linalowasibu katika kambi hiyo ni wananchi wamevamia eneo hilo la serikali lenye hekari 5,500 na kuanza kufanya shughuli.



Vikosi maalum pamoja na mbwa vikiingia katika Kituo cha Polisi cha Kanda Maalum Dar es Salaam jana kwa ajili ya kupanga kuimarisha ulinzi katika kipindi cha mkesha wa Sikukuu ya Mwaka Mpya. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# RC Mara awahakikishia ushirikiano wanahabari

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari katika mwaka 2024 mkoani humo ili waendelee kutangaza miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki mjini Musoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kwa lengo la kuwapongeza kwa ushirikiano wao waliutoa kwake kwa mwaka 2023.

"Ninawapongeza wanahabari wote kwa kazi nzuri mlizofanya kwa mwaka 2023 na ninawaahidi kuwapa ushirikiano zaidi mwaka 2024," alisema Mtanda.

Aliwaagiza pia maofisa habari mkoani humo kuiga mfano huo wa kushirikiana na waandishi.

"Maofisa habari kuweni na ushirikiano chanya na waandishi wa habari ili wananachi waweze kupata taarifa mbalimbali za shughuli za maendeleo zinazofanya na serikali yao," alisema.

Alisema serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kila mkoa na kwamba wananchi wanatakiwa kupata taarifa za miradi hiyo jinsi inavyotekelezwa.

Alifafanua kuwa waandishi ni watu muhimu katika kuwafikishia wananchi taarifa na kwamba maofisa habari katika halmashauri za mkoa huo wasiwe kikwazo kwa waandishi kutekeleza majukumu yao.

"Maofisa habari msiwe kikwazo, shirikianeni na waandishi ili wananchi wapate taarifa zote muhimu za maendeleo ya mkoa wetu, kwani bila wao inakuwa vigumu wananchi kujua kile kinachoendelea mkoani kwao," alisema.

Alisema sio jambo jema pindi waandishi wanapokwenda kwa ofisa habari kwa ajili ya kupata taarifa muhimu za shughuli mbalimbali za maendeleo zinazotekelezwa mkoani humo na kukosa ushirikiano.

Mtanda alisema ni muhimu waandishi wapate ushirikiano ili waendelee kufanya kazi zao kwa uhuru bila vikwazo.

# Watoto wamwombea dua Rais kwa misaada

**Na Mashaka Mgeta**

WAZEE na watoto wenye uhitaji maalum mkoani Tanga, wamemwombea dua Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kupewa msaada wa chakula, mifugo na sabuni.

Zawadi hizo ni mchele, mafuta ya kupikia, mbuzi, sukari, chumvi na sabuni ambavyo vilisambazwa kwa walengwa hao katika ngazi za halmashauri za jiji, miji na wilaya kupitia kwa wakuu wa wilaya.

Katika hitimisho la usambazaji wa zawadi hizo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, aligawa kwenye vituo vitano vya wahitaji hao vya Mwazange, Casa Famiglia, Casa Della Gioia, Abu-Abdulrahman na Goodwill vilivyopo katika Jiji la Tanga.

Wakizungumza baada ya kupokea zawadi hizo, wawakilishi wa wahitaji kutoka makundi maalum ya wazee na watoto walisema kitendo hicho cha Rais Samia ni miongoni mwa ishara zinazodhihirisha namna kiongozi mkuu wa nchi anavyowafikia wananchi wa kawaida kwa nyakati zote.

"Rais Samia angeweza kufanya jambo lingine kuonyesha kuwa anaukaribisha mwaka mpya, lakini kwa kutukumbuka kwake na kutuletea chakula hiki ni jambo linalotufanya tuendelee kumwombea dua njema," anasema mtoto Mary Dustan wa Kituo cha Casa Famiglia.

Mwenyekiti katika kituo cha kulelea wazee cha Mwanzange, Ismail Rashid, alisema kwa vile hakuna wenye nia ovu wanaokosekana dhidi ya watenda mema, dua za wazee wa kituo hicho siku zote ni kwa Rais Dk. Samia ili azidi kuliongoza taifa kwa amani na salama.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Kindamba, alitoa salamu za Rais Samia kwa makundi hayo yakiwa ni sehemu ya Watanzania wanaosubiri na kuomba neema za Mwenyezi Mungu kuingia mwaka 2024.

Alisema zawadi hizo zimetokana na mapenzi ya kweli ya Rais Samia kwa Watanzania wote, pasipo ubaguzi wa aina yoyote.

Kindamba aliwahimiza wananchi kuendeleza masikilizano, utulivu na amani nchini ili kunufaika na mazingira bora yanayochangia kasi ya maendeleo na ustawi wa wananchi, chini ya uongozi wa Rais Samia.



HABARI KIMATAIFA

## Korea Kaskazini kurusha satelaiti tatu 2024

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

KOREA Kaskazini inapanga kurusha satelaiti nyingine tatu za kijasusi mwaka ujao kama sehemu ya juhudi za kuimarisha jeshi lake.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya serikali ya nchi hiyo mwezi uliopita Pyongyang iliweka satelaiti ya kijasusi angani na inadai kuwa tangu wakati huo imepiga picha maeneo makubwa ya kijeshi ya Marekani na Korea Kusini.

Akielezea malengo yake ya 2024, Kiongozi wa Taifa hilo, Kim Jong Un pia alisema kuwa shughuli zake na Korea Kusini zitapata mabadiliko ya kimsingi.

Pia alisema hakuwa na namna ila kusonga mbele na matarajio yake ya nyuklia.

Akizungumza katika mkutano wa mwisho wa mwaka wa Chama Tawala cha Wafanyakazi cha Korea, Kim alisema kuungana na Korea Kusini sasa haiwezekani tena.

Alisema Seoul inachukulia nchi yake kama adui. Huku ikielezwa kuwa ni mara ya kwanza kwa Kim kusema jambo kama hilo na kuashiria mabadiliko rasmi katika sera, ingawa kiutendaji kumekuwa na matarajio madogo ya kuungana kwa miaka kadhaa, bila mafanikio na juhudi kidogo kufanywa.

Taarifa zinaeleza kuwa hadi sasa uhusiano kati ya nchi hizo mbili uko katika hali mbaya.

Mwezi uliopita, baada ya kurushwa kwa satelaiti ya kijasusi, Pyongyang ilivunja makubaliano na Seoul ambayo yalilenga kupunguza mvutano wa kijeshi.

Korea Kaskazini pia iliendelea na majaribio ya mara kwa mara ya makombora yake mwaka mzima wa 2023 na mapema mwezi Desemba ilirusha kombora lake la juu zaidi la masafa marefu na kukaidi vikwazo vya Umoja wa Mataifa.

Kurushwa kwa kombora la balestiki linalovuka mabara, ambalo lina masafa ya kufika katika bara la Amerika Kaskazini, kulizua shutuma za mara moja kutoka Magharibi.

Wakati huo huo Korea Kaskazini haijafurahishwa na Korea Kusini kuimarisha ushirikiano wa kiulinzi na Marekani, baada ya manowari ya Marekani yenye silaha za nyuklia kufika katika maji yake. **BBC**

# 'Uhalifu hautapita bila kuadhibiwa'

**MOSCOW,** RUSSIA

WIZARA ya Ulinzi ya Russia imesema Ukraine imefanya mashambulizi nchini humo kwa roketi za Vampire na kwamba mifumo ya ulinzi wa anga ilinasa makombora yote na baadhi ya roketi hizo, huku ikiahidi kulipiza kisasi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo roketi kadhaa na sehemu za makundi kutoka kwa makombora ya Vilkha yaliyoanguka yalipiga jiji la Belgorod.

Ilisema watu 12 na watoto wawili waliuawa katika mashambulizi hayo, huku wengine 108 wakijeruhiwa.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa ikiwa makombora ya Vilkha yatalenga shabaha zao moja kwa moja na kutoa mabomu ya vishada, matokeo yatakuwa makubwa zaidi.

"Utawala wa Kyiv, ambao ulifanya uhalifu huu, unajaribu kutuvuruga baada ya kushindwa katika mstari wa mbele, na sasa unataka kutuchokoza nyumbani.

"Vikosi vya Russia vinalenga tu vifaa vya kijeshi na miundombinu na tutaendelea kufanya hivyo. Uhalifu huu hautapita bila kuadhibiwa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, ilielezwa kuwa Ukraine bado haijatoa tamko la moja kwa moja kuhusu hali ya Belgorod, lakini vyombo vya habari vya nchini humo vinavyonukuu taarifa za kijasusi vinasema ni shabaha za kijeshi pekee ndizo zilizoshambuliwa.

Hata hivyo, maofisa wa Russia walisema

Ukraine ilifanya msururu wa mashambulizi ya anga katika maeneo ya kusini magharibi mwa Russia juzi.

Ilielezwa kuwa mashambulizi hayo yanafuatia mashambulizi ya Russia dhidi ya Ukraine na kusababisha vifo vya watu 39.

Mashambulizi hayo yalitajwa na Kyiv kama shambulio kubwa zaidi la makombora kufanywa na Russia katika vita vyake dhidi ya Ukraine.

Vyombo vya habari vya Ukraine vikinukuu vyanzo vya kijasusi vikisema kwamba zaidi ya droni 70 zilitumiwa katika msururu wa mashambulizi dhidi ya Russia na ni kambi za kijeshi pekee ndio zilishambuliwa.

Waliongeza kuwa ndege zisizo na rubani zilifanikiwa kugonga kiwanda cha kielektroniki katika mkoa wa Bryansk kinachotumika kutengeneza vifaa vya kijeshi vya Russia kama vile makombora ya masafa marefu na mifumo ya kuzuia ndege. **BBC**



Raia wa Palestina akilia baada ya familia yake kudhuriwa na shambulio la Israel juzi. **PICHA MTANDAO**

# Taasisi za Palestina kuandamana Washington

**GAZA,** PALESTINA

TAASISI za Kutetea Haki za Binadamu za nchini Palestina, zinazofanya kazi nchini Marekani zimetangaza kuwa ziko tayari kuandaa wiki ya maandamano ili kushinikiza kusitishwa mara moja kwa hujuma za Israel dhidi ya Ukanda wa Gaza.

Hayo yalibainishwa jana na shirika la habari la WAFA la Palestina, na kuangoza kuwa taasisi hizo zinajiandaa kuzindua matukio kutoka siku

ya kwanza ya mwaka mpya, hadi Januari 7, 2024.

Ilieleza kuwa hilo litafanyika kwa lengo la

kutuma ujumbe kwa utawala wa Marekani kuhusu haja ya kuingilia kati ili kukomesha vita hivyo na kuzuia mauaji ya watu wasio na hatia.

"Kupitia Wiki ya Kitaifa kote Marekani, taasisi hizo zinatoa wito wa kuunga mkono uhuru wa Palestina, kukomesha mauaji ya kimbari ya Israel, kukomesha misaada ya Marekani kwa

Israel, kuondoa mzingiro wa Gaza na

kukomesha uvamizi wa Israel na ukoloni wake kwa ardhi za Wapalestina na Waarabu," shirika hilo lilisema.

Hata hivyo ilielezwa kuwa Israel imeendelea kufanya uvamizi huko Gaza na kusababisha makumi ya vifo, huku chanzo cha hospitali kikibainisha kwamba uvamizi wa Israel wa

juzi ulisababisha vifo vya watu wasiopungua 64 na kujeruhi zaidi ya watu 186.

**RFI**

# Rwanda yakanusha kuwafadhili waasi wa Burundi

**KIGALI,** RWANDA

RWANDA imekanusha matamshi ya Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, yaliyodai kuwa serikali mjini Kigali inawafadhili waasi wanaoendesha hujuma dhidi ya Burundi.

Waasi hao ni wa Red Tabara wanaoendesha hujuma dhidi ya Burundi kutokea ardhi ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (**DRC**).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na serikali ya Rwanda, matamshi hayo ya Rais Ndayishimiye hayana ukweli na kwamba nchi hiyo haina mahusiano na kundi lolote la wabeba silaha linaloiandama Burundi.

Siku chache zilizopita Rais Ndayishimiye aliituhumu Rwanda kuwasaidia kwa hali na mali waasi wa Red Tabara, tuhuma zinazozidisha uhasama kati ya mataifa hayo jirani na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aidha, serikali ya Rwanda ilikumbusha kuwa hivi karibuni, iliwakabidhi kwa Burundi wanamgambo walioingia Rwanda hii ikiwa kudhihirisha azma ya ushirikiano na jirani yake huku ikiwataka viongozi wa Bujumbura kuwasilisha malalamiko yao kwa njia za kidiplomasia ili yapatiwe suluhu la kirafiki.

Hata hivyo Rais Ndayishimiye alielezea masikitiko yake kwamba juhudi zote za majadiliano na Rwanda juu ya suala hilo hazijazaa matunda. **DW**

# CCM TANGA YABAINI UPIGAJI JENERETA UWANJA MKWAKWANI

**Na Hamida Kamchalla, TANGA**

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdalla, ameushukia uongozi wa Uwanja Mkwakwani jijini hapa, kwa tuhuma za upigaji wa fedha za manunuzi ya jenereta la kuwashia taa kwa ajili ya mechi zinazopangwa kucheza nyakati za usiku.

Akizungumza na wadau wa michezo mkoani hapa na viongozi wa Klabu za Coastal Union na African Sports, ikiwa ni pamoja na kusikiliza kero mbalimbali kuhusu soka, mwenyekiti huyo alisema kuna ubabaishaji katika ununuzi wa jenereta hilo kwani fedha alizotoa zilikuwa za kununua jipya, lakini cha kushangaza limenunuliwa lililotumika.

"Nilikabidhi Sh. milioni 30 kwa ajili ya kununulia jenereta jipya ili lifungwe uwanjani timu zetu ziweze kucheza mpira hata usiku, leo mnaniambia mmenunua lililotumika, haiwezekani.

"Wale wote walioniingiza mkenge kwenye ununuzi wa jenereta watawajibika, kwenye fedha za chama sitacheka na mtu. Chama kinahitaji fedha ili kiweze kwenda na kuweka imani yake kwa wanachama wake," alisema.

Aidha, alisema tayari amepokea taarifa kuhusu jenereta hilo kutokufanya kazi.

Mwenyekiti huyo alisema alitoa fedha hizo ili kununuliwa jenereta jipya huku akionesha kushangazwa na taarifa ya kuharibika katika muda mfupi, huku akimtaka meneja wa uwanja huo kutoa ufafanuzi wa suala hilo mbele ya wadau waliohudhuria katika mkutano huo.

Akitoa ufafanuzi huo, Meneja wa Uwanja wa CCM Mkwakwani, Nasser Makau, alisema jenereta hilo ni bovu na linatakiwa kufanyiwa marekebisho ya kina kwa kuwa halikuwa jipya.

"Mheshimiwa mwenyekiti jenereta linahitaji kufanyiwa 'Overhaul'... halikuwa jipya limenunuliwa likiwa limeshatumika," alisema Makau.

Hata hivyo, majibu hayo yalionekana kutomridhisha mwenyekiti huyo, ambapo alimwagiza Katibu wa CCM Mkoa wa Tanga, Selemani Sankwa, kufuatilia kwa ukaribu na kutoa taarifa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa, ili kubaini ubadhirifu wote uliofanywa huku akidai hatomsamehe yeyote aliyehusika katika sakata hilo.

"Huu ni upigaji na hali hii inasababisha kurudisha nyuma maendeleo ya soka mkoani kwetu, katibu fuatilia hili na utoe taarifa kwa RPC ili uchunguzi ufanyike" alibainisha.

Mbali na hayo, pia mwenyekiti huyo alikabidhi fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni 20 kwa klabu ya Coastal Union na African Sports kila moja ikiondoka na Sh. milioni 10 huku akiahidi kukabidhi kiasi kama hicho tena baada ya siku chache.

"Ili kuendelea kuzisaidia klabu zetu ambazo ndizo kubwa hapa jijini kwetu, mimi nitachangia Sh. milioni 20 kwa kila klabu na leo nitakabidhi Sh. milioni 10 kwa kila moja, nyingine ataziwasilisha katibu wangu baada ya siku mbili tatu hizi, hii ni kwa ajili ya kuendelea kuziunga mkono na kusaidiana katika soka letu," alisema.

**NI SHIDA...**



Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, katika harakati za kuitafutia timu yake bao dhidi ya mabeki wa Nottingham Forest, wakati United ikikubali kichapo cha mabao 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja The City Ground juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga Princess yatamba kuimarika ushambuliaji

**Na Saada Akida**

BAADA ya kucheza mechi mbili za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, amesema safu yake ya ushambuliaji imeimarika na sasa wanajiandaa vizuri kuelekea mchezo wa 'Derby' dhidi ya Simba Queens.

Yanga Princess walicheza mechi ya kwanza na kushinda mabao 2-0 dhidi ya Baobab Queens na mchezo wa pili Amani Queens 6-1, ambapo sasa mechi yao ijayo ni dhidi ya Simba Queens itakayopigwa keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi, Dar es Salaam. Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Haalubono alisema anafurahi kuona kikosi chake kinaimarika na kupata muunganiko mzuri hasa kwenye safu yake ya ushambuliaji.

Alisema awali walikuwa na tatizo kwenye safu ya ushambuliaji ambapo walishindwa kufanya vizuri katika michezo ya Ngao ya Jamii na kumaliza nafasi ya tatu, lakini walifanyia kazi na kuonekana kuimarika katika michezo miwili ya ligi na kufunga jumla ya mabao nane.

"Kikosi kimeanza kuimarika, ukiangalia katika mechi nne za ushindani tulizocheza ikiwamo Ngao ya Jamii na Ligi Kuu unaona vijana wangu wanazidi kuwa imara na muunganiko unakuwa mzuri.

"Tumefanikiwa kufunga mabao nane katika mechi mbili za ligi pia kuruhusu bao moja, unaona jinsi ambavyo safu ya ushambuliaji inakuwa imara, tunatarajia kuwa bora zaidi mchezo wetu ujao dhidi ya Simba Queens," alisema Haalubono.

Kuhusu mchezo wa derby, alisema hautakuwa rahisi kwa sababu wamewahi kukutana mara moja ndani ya msimu huu na kutolewa kwa mikwaju ya penalti na sasa wamejipanga kuhakikisha wanavuna alama muhimu mbele ya watani wao.

## Mlandege mambo magumu kutetea Mapinduzi Cup

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

NDOTO ya Mabingwa Watetezi wa Kombe la Mapinduzi, Mlandege FC, kutetea taji lao zinaendelea kuota mbawa baada ya kutoka sare michezo miwili mfululizo msimu huu.

Mlandege FC juzi katika mchezo wao wa pili walilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Vital'O ya Burundi mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Amaan Complex majira ya saa 10 alasiri.

Katika mechi hiyo Mlandege ilikuwa ya kwanza kuzifumania nyavu za wapinzani dakika ya 45 kupitia Optatus Lupekenya, wakati Vital'O walibidi kusubiri hadi dakika ya 64 kuweza kusawazisha, shukrani zikimwendea Kessy Jordan aliyeinusuru kuzama.

Mlandege sasa imebakisha mchezo mmoja dhidi ya Chipukizi FC wa kukamilisha hatua ya makundi utakaopigwa Alhamisi wiki hii.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Mlandege, Jaala Abdallah, alisema mchezo mmoja uliobaki kwao wao watacheza kama fainali ili kuweza kusonga mbele.

Alisema licha ya kuambulia alama mbili katika michezo miwili, lakini matarajio yake ni kuhakikisha timu hiyo inapata alama tatu katika mchezo wao wa mwisho.

Abdallah alisema si kama timu yake haichezi vizuri, bali kwa mwaka huu timu zote zimejiimarisha vizuri na ushindani umeongezeka hasa kwa kuwapo kwa klabu kutoka nje ya Tanzania.

"Tunahitaji mchezo wa mwisho kupambana kwa hali ya juu ili kuhakikisha tunashinda ili tuwe na uwezekano mkubwa wa kusonga mbele katika michuano hii ambayo mwaka huu ushindani umeongezeka zaidi," alisema.

Hata hivyo, alisema mchezo wao wa mwisho dhidi ya Chipukizi utakuwa mgumu kwa kuwa timu hizo zimekutana kwenye Ligi Kuu Zanzibar, hivyo zinajuana vizuri.

"Mara nyingi unapokutana na mpinzani unaejuana naye vizuri mchezo unakuwa mgumu kwa kuwa tayari mshasomana mbinu zenu, hivyo wachezaji wanatakiwa wawe na uwezo wa kutosha ili kupata matokeo mazuri," alisema.

Kocha wa Vital'O, Sabaho Tarib, alisema timu yake ilicheza vizuri, lakini kukosa umakini ndiko kulikosababisha kushindwa kutoka na ushindi.

Alisema ana matumaini makubwa mchezo wake wa mwisho wa hatua hiyo ya makundi dhidi ya Azam FC kesho, watapata alama tatu kwani wachezaji wake wamebadilika na wanacheza kwa malengo ya kupata ushindi.

ZISIKUPITE

### SPURS YAMTAKA DRAGUSIN

KLABU ya Tottenham Hotspur inajipanga kuwasilisha ombi la kumnunua beki wa Genoa kutoka Romania, Radu Dragusin, huku wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, akisema anataka kuhama. **(SportItalia)**

### TODIBO AOTA MBAWA

TOTTENHAM Hotspur wameelekeza mawazo yao kwa Radu Dragusin kwa sababu ya uwezekano wa kumnunua beki wa kati wa Nice, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 24, unaelekea kushindikana. **(Fabrizio Romano)**

### ALLEGRI HAMTAKI PHILLIPS

KOCHA wa Juventus, Max Allegri, huenda akapinga hatua ya klabu hiyo kumnunua Kalvin Phillips wa Manchester City kwa sababu hafikirii kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 28, anafaa mfumo wake wa kimbinu**. (Calciomercato)**

### BARCA NA GREENWOOD

KLABU ya Barcelona haina uwezekano wa kumnunua Mason Greenwood kwa sababu hawawezi kumudu thamani ya pauni milioni 40 inayotakiwa na Manchester United kwa mshambuliaji huyo wa Kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu nyingine ya LaLiga, Getafe**. (Sport)**

### ATLETICO WAJITOSA RASMI

ATLETICO Madrid tayari wameweka mikakati ya awali juu ya uwezekano wa kumnunua Mason Greenwood, 22. **(Marca)**

### VARANE APELEKWA SOKONI

KLABU ya Manchester United iko tayari kupokea ofa Januari hii kwa ajili ya mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane, 30. **(Football Insider)**

### DIAO ATAJWA BRENTFORD

KLABU ya Brentford inatazamiwa kuwasilisha ofa kiasi cha euro milioni 30 kwa winga wa Real Betis, Assane Diao, ambacho kinakaribiana na kifungu cha kutolewa cha mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 18. **(Diario de Sevilla)**

### LINDELOF KUONGEZEWA

KLABU ya Manchester United imeanzisha mchakato wa kuongeza mkataba wa beki wa Sweden, Victor Lindelof hadi Juni 2025. Mkataba wa awali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ulipaswa kumalizika msimu huu wa majira ya joto. **(Athletic)**

### MAATSEN ATAKIWA DORTMUND

BORUSSIA Dortmund Januari hii ina nia ya kumsajili mlinzi wa pembeni wa Chelsea, Ian Maatsen, 21. **(Voetbal international)**

### ROBERTSON AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton inafuatilia maendeleo ya kiungo wa kati wa Manchester City na Australia mwenye umri wa miaka 20, Alex Robertson, ambaye yuko kwa mkopo wa msimu mmoja pale Portsmouth. **(The news)**

### NINO KUTUA FOREST

NOTTINGHAM Forest inatumai kukamilisha dili la pauni milioni sita kwa mlinzi wa kati wa Fluminense, Mbrazil Nino mwenye umri wa miaka 26, Januari hii na wako kwenye mazungumzo ya juu na Monaco kuhusu kumnunua winga huyo wa Ureno, Gelson Martins, 28. **(Mirror)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AMALIZA 2023 MFUNGAJI BORA DUNIANI

Awapiku Mbappe, Kane na Haaland, asema atasema itakapokamili...

**RIYADH, Saudi Aarabia**

CRISTIANO Ronaldo amemaliza mwaka 2023 akiwa mfungaji bora zaidi duniani baada ya kufunga bao lake la 54 katika ushindi wa 4-1 wa Al Nassr dhidi ya Al Taawoun kwenye Ligi ya Saudia Jumamosi.

Mabao 54 ya fowadi huyo wa Ureno katika mashindano rasmi ya klabu na nchi yalikuja katika mechi 59 na kuwashinda Harry Kane wa Bayern wa Munich na Kylian Mbappe wa Paris Saint-Germain (wenye 52) pamoja na nyota wa Manchester City, Erling Haaland (50).

Ni mara ya tano kwa Ronaldo kumaliza mwaka akiwa mfungaji bora wa dunia, baada ya kufanya hivyo mwaka 2011, 2013, 2014 na 2015 akiwa Real Madrid.

Mabao yake 54 ndiyo mengi zaidi kwa Ronaldo kufunga kwa mwaka mmoja tangu afunge mabao 55 mwaka 2016, aliposhinda moja ya tuzo zake tano za Ballon d'Or.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alijibu mafanikio hayo kwa chapisho kwenye Instagram, akiandika: "54 - nitasema itakapokamilika! Asante, timu."

Bao la Jumamosi la Ronaldo lilipatikana katika kumbukumbu ya mwaka mmoja tangu ajiunge na Klabu ya Al Nassr ya Saudia baada ya kuondoka kwa utata pale Manchester United.

Al Nassr walikuwa wanaongoza 3-1 kupitia mabao ya Marcelo Brozovic, Aymeric Laporte na Otavio wakati Ronaldo alipofunga kwa kichwa kutoka umbali wa yadi sita dakika ya pili ya muda wa majeruhi.

Lilikuwa bao lake la 20 katika mechi 18 za Ligi ya Saudia hadi sasa msimu huu.

Kwa ushindi huo, Al Nassr wamebakia katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi ya Saudia, wakiwa na pointi 46 katika michezo 19, pointi saba nyuma ya viongozi Al Hilal.

# TEN HAG: NI MIMI TU NAWEZA KUMALIZA UGUMU WA UNITED



**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag amesema yeye ndiye mtu sahihi wa kuiongoza Manchester United kutoka katika hali mbaya ya matokeo ya sasa baada ya kuambulia kichapo cha tisa kutoka kwa Nottingham Forest kwenye Ligi Kuu ya England, Jumamosi.

United ipo nyuma kwa pointi tisa kutoka kwenye nafasi nne za juu na haipo kwenye nafasi za mashindano ya Ulaya wanapouanza mwaka 2024.

Klabu hiyo pia itafanyiwa mabadiliko ya mfumo wa soka baada ya Kampuni ya INEOS itakapokamilisha uwekezaji wao wa hisa za asilimia 25 kwa kuidhinishwa wiki chache zijazo.

Mkurugenzi wa Masuala ya Soka wa INEOS, Dave Brailsford, ambaye atakuwa kwenye bodi ya soka ya watu watatu dili hilo litakapokamilika, aliitazama United ikichapwa mabao 2-1 na Forest, lakini Ten Hag ana imani kuwa anaweza kuiongoza timu hiyo kutoka katika kipindi kigumu.

„Bila shaka, (INEOS) wananifahamu na wanajua ninapokuwa na kikosi kile chenye njaa ya matokeo basi matokeo yatapatikana," alisema Ten Hag.

„Tayari tumethibitisha dhidi ya timu za juu kwamba tunaweza kwenda kichwa mbele.

„Nina hakika na nina imani kubwa kwamba tunaweza kupata maendeleo katika timu hii na kupata uthabiti zaidi kuliko wakati huu. Ni sehemu ya mradi.

„Tulifanya kazi kupita kiasi mwaka jana, mwaka huu - hadi sasa hatufanyi vizuri na tunapaswa kufanya vizuri zaidi. Lazima tuongeze kasi. Ni lazima niongoze mchakato huo.

„Najua wachezaji (waliomajeruhi) wanaporejea, nina uhakika upande huu utakuwa na nguvu zaidi. Unapaswa kuwa wazi."

Kikosi cha Ten Hag pia kilipata suluhu dhidi ya Liverpool mwezi uliopita, na kuwa timu pekee kuepuka kufungwa kwenye Uwanja wa Anfield dhidi ya timu ya Jurgen Klopp kwenye ligi msimu huu kabla ya Arsenal kutoka sare ya 2-2 wiki iliyopita.

Na Ten Hag alikiri kwamba kutofautiana ni tatizo kubwa ambalo upande wake lazima ushinde.

„Jambo moja liko wazi, hatuko thabiti," alisema. „Tunaweza kuzishinda timu bora kwenye ligi lakini pia tunapoteza dhidi ya zingine."

# Lloris rasmi sasa atua Los Angeles

**CALIFORNIA, Marekani**

HUGO Lloris ameondoka rasmi katika Klabu ya Tottenham Hotspur na kujiunga na Klabu ya Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), Los Angeles FC.

Kipa huyo namba moja wa zamani wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 37, alitumia zaidi ya miaka 11 na timu hiyo ya Kaskazini mwa London baada ya kujiunga nayo kutoka Lyon mnamo Agosti 2012, akicheza mechi 151 bila kuruhusu bao katika mechi 447 kwenye mashindano yote.

Lloris pia alifurahia mafanikio makubwa akiwa na Timu ya Taifa ya Ufaransa, ‚Les Bleus', akinyanyua taji la Kombe la Dunia kama nahodha mwaka 2018 kabla ya kustaafu soka la kimataifa Januari iliyopita na sasa ataendelea na kazi yake nzuri huko California.

Rais mwenza wa Los Angeles na Meneja Mkuu, John Thorrington, alisema: „Hugo bila shaka ndiye kipa aliyefanikiwa zaidi wa kizazi chake na mshindi aliyethibitishwa.

„Tunafurahi sana kwamba Hugo amechagua LAFC kwa awamu inayofuata ya kazi yake nzuri.

"Analeta uzoefu wa uongozi usio na kifani katika viwango vya juu vya soka, jambo ambalo tunajua litainufaisha sana klabu yetu katika harakati zetu za kusaka mataji zaidi.

„Ningependa kuwashukuru Tottenham kwa ushirikiano wao, na ninaungana na Los Angeles yote kuwakaribisha Hugo, mkewe Maine, na watoto wao watatu hapa LAFC."

Spurs walimpongeza Lloris kwa taarifa yao wenyewe, wakimtaja kipa huyo kuwa mmoja wa „watumishi bora wa klabu".

Klabu hiyo ya London Kaskazini iliongeza: „Tunamtakia Hugo na familia yake kila la kheri kwa siku zijazo.

„Tutakusanyika ili kumshukuru Hugo ana kwa ana wakati wa mapumziko kwenye mechi ya Jumapili (jana) dhidi ya Bournemouth kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur.

Lloris hakuwa ameichezea Spurs tangu ilipopoteza kwa mabao 6-1 dhidi ya Newcastle Aprili 2022 na kipa aliyesajiliwa majira ya joto, Guglielmo Vicario akiwa chaguo la kwanza kwa kocha Ange Postecoglou.

# Rodri asifu kiwango cha Foden

**MANCHESTER, England**

RODRI amemmwagia sifa mchezaji mwenzake, Phil Foden baada ya nyota huyo wa Kimataifa wa England kuiongoza Manchester City kuishinda Sheffield United kwenye mchezo wa Ligi Kuu, Jumamosi.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23, alisaidia mabao yote mawili wakati mabingwa hao watetezi walipoibuka na ushindi wa 2-0 wakiwa kwenye dimba la Etihad, huku Rodri akinufaika na usaidizi wa mwenzake kwa kufumania nyavu kwa mara ya kwanza kwenye dimba la nyumbani tangu Februari mwaka jana.

Julian Alvarez pia alifunga bao wakati kikosi cha Pep Guardiola kikisonga mbele ya Arsenal kwenye msimamo wa ligi.

Kwa bao lake, Rodri aliiambia Sky Sports: „Nilifikiri Phil (Foden) angeweza kunielekeza na kisha kusema ukweli sikuwa na nia ya kupiga shuti.

„Phil ana uwezo wa ajabu wa kugeuka kwa kasi kiasi hicho. Ana ustadi huu na akiwa na mpira anaweza kugeuka haraka.

„Ilitubidi kuwa na subira, lakini tunapoweza kupata pasi hii yeye ni mbadilishaji. Anaongeza kasi anayoweza kupiga na kupiga pasi."

Rodri pia alisisitiza umuhimu wa City kujifunza kutokana na makosa yao dhidi ya Crystal Palace, waliposalimisha uongozi wa 2-0 Etihad na kutoka sare ya 2-2.

Mhispania huyo aliongeza: „Tulijifunza kutoka mechi ya mwisho dhidi ya Crystal Palace, hisia sawa za mchezo, kudhibiti, lakini mwisho walipata nafasi na tukatoka sare.

„Ilitubidi kuendelea kuzingatia na wao (Sheff Utd) hawakuwa na nia ya kuja kwetu kwa hiyo muhimu kwetu ni ushindi huu."



HABARI MICHEZO

# SINGIDA FG, APR, SIMBA VITANI MAPINDUZI CUP

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MTIFUANO mkali unatarajiwa kushuhudiwa leo katika michuano ya Kombe la Mapinduzi wakati ‚Wakulima wa Alizeti', Singida Fountain Gate, watakaposhuka Uwanja wa Amani Complex visiwani hapa kuvaana na Miamba ya Soka ya Rwanda, APR FC.

Mchezo huo utapigwa majira ya saa kumi alasiri wakati saa mbili usiku JKU SC wataikaribisha Klabu ya Simba.

Singida Fountain Gate tayari wamevuna alama tatu kutoka kwa vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU SC katika mchezo wake wa Kwanza uliochezwa Ijumaa iliyopita wakati wapinzani wao APR FC wao wakitupa karata yao ya kwanza katika michuano hiyo.

Wakizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana, makocha wa timu hizo, kila mmoja alisema wanataka kupata alama tatu ili kuweza kusonga mbele kwenye mashindano hayo.

Kocha wa APR, Thierry Froger, alisema matarajio yake ni kuona anafanya vizuri katika mashindano hayo na hatimaye kunyakuwa ubingwa ingawa ni mashindano ambayo ratiba imebana.

Alisema japo wamekuja kushindana, tatizo timu inapata masaa machache ya kupumzika jambo ambalo litasababisha wachezaji wake kuchoka.

"Timu inapumzika siku moja halafu siku ya pili mechi, hii haiko vizuri maana itakuwa wachezaji bado hawajakuwa vizuri kutokana na mchezo waliomaliza, hivyo ratiba inabana sana," alisema.

Kocha wa Singida Fountain Gate, Thabo Senong, alisema kwa mwaka huu matarajio yake ni kuhakikisha wanachukua ubingwa baada ya mwaka 2023 kushindwa kufanya hivyo na kumaliza nafasi ya pili.

Alisema wanakabiliwa na mchezo mgumu dhidi ya APR, timu ambayo inafanya vizuri katika Ligi Kuu ya Rwanda, hivyo lazima wachezaji wazingatie nini wanahitaji ili waweze kupata ushindi katika mchezo huu.

"Awali nilishasema kwamba katika mashindano haya matarajio ni kuona tunafanya vizuri ikiwamo kushinda michezo yetu yote katika hatua ya makundi, lakini mchezo uliombele yetu kwetu sisi mgumu, hivyo lazima tuwe na tahadhari ili kutimiza lengo letu," alisema.

Hata hivyo, alisema wachezaji wake wanapaswa kuzingatia kuwa wanaenda kucheza na timu kubwa na yenye wachezaji wazuri wenye uzoefu wa mashindano makubwa.




Wachezaji wa Simba wakiwasili visiwani Zanzibar jana tayari kwa michuano ya Kombe la Mapinduzi ambapo leo usiku watashuka Uwanja wa Amaan Complex kuvaana na JKU. **PICHA: SIMBA**

# Kipre Junior mchezaji bora Desemba

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Kipre Junior, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Desemba wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24.

Kocha Mkuu wa Timu ya Azam, Bruno Ferry, pia amechaguliwa kuwa ndiye kocha bora wa mwezi huo wa mwaka jana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), ni kwamba washindi hao wamechaguliwa na Kamati ya Tuzo iliyo chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF).

Taarifa hiyo imesema kuwa Kipre, ambaye hucheza kama winga, amemshinda mchezaji mwenzake wa Azam, Prince Dube, pamoja na kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki ambao aliingia nao fainali.

Kwa mwezi huo, Kipre alionesha kiwango kikubwa na kuisaidia timu yake kupata ushindi katika mechi zote tatu, akihusika na mabao manne kwa dakika 235 alizocheza.

Kwa upande wa Kocha Bruno, ameshinda tuzo kwa kuiongoza timu yake ya Azam kushinda mechi zote tatu za Desemba, ikiichana KMC mabao 5-0, JKT Tanzania 2-1, na Kagera Sugar 4-0, ikipanda kutoka nafasi ya pili hadi ya kwanza.

Aliwashinda makocha wenzake, Miguel Gamondi wa Yanga na Ahmad Ally wa Prisons.

Mbali ya takwimu hizo, kwa mujibu wa takwimu za Nipashe, Kipre, raia wa Ivory Coast, ndiye anayeongoza kwa ‚assist' mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, akiwa amefanya hivyo mara sita, akifunga mabao manne, hivyo kuhusika katika mabao 10 kati ya 35 ambayo Azam imefunga.

Kamati hiyo pia imemchagua Meneja wa Uwanja wa Azam Complex, Amir Juma, kuwa Meneja bora wa uwanja kwa mwezi huo.

## Ngoma kuletewa 'mtu na nusu' Simba

INATOKA UK. 24

baadhi ya nyota wakawahi michuano ya Kombe la Mapinduzi na kuonekana katika baadhi ya mechi.

Aliongeza kuwa hawana kikosi kibaya bali kuna mambo madogo ambayo Kocha Benchikha atayafanyia kazi ikiwamo kujitoa kwa wachezaji na kupambana, hilo amekuwa akilihimiza katika mazoezi yao.

Ahmed alisema kikosi kiliwasili visiwani Zanzibar jana salama na wako tayari kwa michuano hiyo na leo wanashuka dimbani kukabiliana na JKU FC.

## Yanga SC yamwahidi Dk. Mwinyi ubingwa

INATOKA UK. 24

Alisema kuwa msimu huu wamekuja kamili zaidi kuliko misimu mingine iliyopita, hii inaonesha kuwa wana dhamira ya dhati ya kutwaa kombe hilo.


„Msimu huu tumekuja na kikosi chetu chote ukilinganisha na misimu iliyopita, isipokuwa wale tu ambao wako kwenye kikosi cha timu ya taifa na wawili watatu ambao wana dharura maalum na hata hivyo hao wenye dharura watarejea na kuungana na kikosi wakati mashindano yanaendelea.

Sisi kwetu michuano hii ni heshima, kuuheshimisha mpira wa Zanzibar na kumpa heshima Rais wa Zanzibar, kwa kutumia fedha nyingi kwenye michezo na matunda yao tunayaona.

Msimu uliopita, Yanga ilitolewa hatua ya makundi, ikimaliza ya pili nyuma ya Singida Big Stars (sasa Singida Fountain Gate) iliyosonga mbele na kwenda moja kwa moja mpaka fainali, lakini ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya Mlandege ambao kwa sasa ndiyo mabingwa watetezi.

Michezo
Jumatatu Januari 1, 2024
Nipashe

Ronaldo amaliza 2023 mfungaji bora duniani UKURASA 21





# NGOMA KULETEWA 'MTU NA NUSU' SIMBA

●●● Uongozi wafunguka kila idara sasa kuongezewa kifaa huku Benchikha akitaka...

**Na Saada Akida**

WAKATI leo wakishuka Uwanja wa Amaan Complex kuvaana na JKU kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi, uongozi wa Klabu ya Simba umeweka wazi kuwa wako sokoni kwa ajili ya kusaka kiungo mkabaji mwenye uwezo mkubwa ambaye atakuja kuleta changamoto kwa Fabrice Ngoma ili kukiimarisha kikosi cha timu hiyo.

Simba haijawa bora kwenye kila maeneo ikiwa pamoja na safu ya ulinzi, ushambuliaji na eneo la kiungo mkabaji ambapo kwa sasa kazi hiyo ipo kwa Ngoma, Sadio Kanoute na Mzamiru Yassin.

Taarifa za uhakika ni kwamba tayari Simba imekamilisha usajili wa nyota wawili Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar ambaye yuko kwenye majukumu na Taifa Stars, Mauricio Cortes kutoka Klabu ya Comerciantes FC ya Colombia huku pia ikimfuatilia beki wa kulia wa Mlandege FC ya Zanzibar, Abdallah Said.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema wakati kikosi chao kimefika salama visiwani Zanzibar kwa ajili ya michezo ya Kombe la Mapinduzi, skauti wako sokoni kufanya usajili na kwenye kila idara kuna aina ya wachezaji ambao wanapaswa kusajiliwa.

Alisema maboresho ya kikosi chao yatafanyika kila idara kwa kuzingatia maeneo muhimu yaliyopendekezwa na Kocha Abdelhak Benchikha ikiwamo kiungo ambaye atatoa ushindi wa kupata nafasi ya kucheza katika kikosi cha timu hiyo.

"Kwenye eneo la kiungo tutaongeza mtu ambaye atakuwa bora kama ilivyo kwa Ngoma kuja kuongeza nguvu ndani ya kikosi kwa sababu tunahitaji kuimarisha na kupata kikosi kipana.

„Tunaimani kubwa na usajili ambao unaendelea kufanywa katika maeneo mengine ambao utaleta tija ndani ya timu, hatufanyi usajili tu bali tunahitaji kuleta watu ambao wataleta ushindani ndani ya kikosi chetu," alisema Ahmed.

Alisema usajili unaoendelea na kuna baadhi ya wachezaji wameshasaini na muda utakapofika watawekwa wazi na huenda

INAENDELEA UK. 23

# Yanga SC yamwahidi Dk. Mwinyi ubingwa

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya Yanga imetamba kuwa hakuna wa kuizuia kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, ambalo watalitoa zawadi kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Yanga ambayo jana usiku ilitarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Jamhuri, imesema kuwa imejiandaa vizuri na kombe hilo linalochezwa Uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar na ubingwa wao watauelekeza moja kwa moja kwa Rais Mwinyi, ikiwa ni zawadi yake kutokana na kufanya kazi kubwa ya kutoa pesa nyingi kwa ajili ya kukarabati Uwanja wa Amaan.

Akizungumza jana mchana kutoka Zanzibar, Makamu wa rais wa klabu hiyo, Arafat Haji, alisema tayari wameshakaa na matawi yote ya Yanga, Zanzibar kupata mikakati ya kuhakikisha kombe linabaki Zanzibar, kwani itakuwa ni aibu kubwa kwa timu hiyo kukosa ubingwa kutokana na kuwa na kikosi bora.

„Tunataka kuchukua ubingwa na kumpatia Rais Mwinyi kama shukrani kwa kuwajengea Wazanzibar viwanja hivi vizuri, unaona nje ya Uwanja wa Amaan pia kuna viwanja vya mazoezi vilivyokarabatiwa vema, lakini katika kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

„Tarehe 29 (Desemba), tulikutana na matawi yote ya Zanzibar na kukubaliana kwamba itakuwa ni aibu kwa Yanga hii iliyokuja msimu huu na uzuri wote katika kusakata kabumbu, halafu tusilichukue Kombe la Mapinduzi. Kwa hiyo tumejipa malengo wadau wa soka Zanzibar kuwa tunaiheshimisha Yanga.

„Tumeongea na Kocha Miguel Gamondi na wachezaji kuwa heshima ya Yanga ipo mikononi mwao na wahakikishe wanailinda kwa kutwaa kombe ili dhamira yetu ya kumpa zawadi Rais itimie," alisema.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042